Kuna Njia Moja Tu Iliyotolewa Na Mungu Kwa Kitu Chochote

Asante, Ndugu Carlson. Ni vyema sana kukutana na wewe, na Bwana akubariki. Habari za jioni, marafiki. Sasa, kabla hatujaketi chini, hebu tuzungumze tu na Mfalme mkuu ambaye sisi sote tupo hapa kumwabudu.

2 Baba yetu wa Mbinguni, tunashukuru kwa ajili ya fursa ya kurudi tena katika mji huu mashuhuri, Chicago, kukutanika hapa pamoja na wale ambao wanakungojea Kuja kwa Bwana Yesu. Pia tunaomba, Baba, kwa kuwa juhudi zetu zimetolewa, katika wote wanaume na wanawake, wavulana na wasichana, kuona uamsho au kuchochewa, labda kuwaita wengine wachache waingie ambao wameachwa nje katika mji. Jalia huu uwe ndio wakati mkuu ambapo yule wa mwisho ataitwa aingie kabla ya hukumu kuipiga nchi hii. Baba, tunaamini kwamba kungali na wengine zaidi wanaongojea, na sisi tunawatafuta. Watume waingie ndani, wakati huu, Baba. Jalia hilo, kwamba waweze kumpokea Kristo, na wahesabiwe miongoni mwa wale wateule ambao watatwaliwa katika ule Unyakuo mkuu ulio katika wakati ujao. Jalia hilo, Bwana.

3 Juhudi hizi tunazotoa, na zimetolewa na Ndugu yetu Carlson na wote hao hapa, kwamba, mahali hapa ambapo wamegeuza kutoka kwa maskini nyumba ya wiski na ulingo wa mwereka, kuwa nyumba ya Bwana. Bwana, jalia iwe ni kumbukumbu na wakilisho la wongofu wa wenye dhambi, kwa Kristo.

4 Tusikie, Baba, katika mambo haya, kuponya wagonjwa na kufanya mambo haya makuu tunayoomba, kwa kuwa ni katika Jina la Yesu Kristo, na kwa ajili ya heshima na utukufu Wake, tunaomba hayo. Amina.

Mwaweza kuketi. Asanteni, sana.

5 Daima ni majaliwa kuja Chicago. Daima nimejisikia hivyo. Sijakuwa hapa kwa muda, kwa sababu siishi hapa tena, ni—ninaishi Arizona, huko Tucson. Na tupo hapa Jeffersonville, kwenye likizo ya majira ya joto, na ninaondoka hapa Jumatatu asubuhi. Na punde tu nifikapo nyumbani, vitu vinaningojea kurudi Tucson tena.

6 Na, lakini, nipo hapa nikitengeneza kanda, Jumbe ambazo ninasambaza kwenye kanda. Naye Bwana amekuwa akitubariki. Jumapili asubuhi tulikuwa na Ujumbe wa saa nne. Sitarajii

kufanya hivyo hapa. Lakini saa nne juu ya ufunuo wenye sehemu tatu wa Yesu Kristo kuwa . . . Siri ya Mungu iliyofichwa tangu msingi wa ulimwengu. Na Bwana kwa hakika alitubariki. Tumekuwa na baraka kuu, na Mungu ameponya wagonjwa miongoni mwetu.

7 Machache, yapata majuma matatu yaliyopita, nilipokuwa nikizungumza, mwanaume akisimama mbele zetu, ninii yake . . . Yeye ni Mwingereza. Mke wake ni Mnorwe. Na yeye ni mwuguzi mzuri sana, na yeye mtu mwema sana. Na kwa hiyo, mwanaume huyo, nilikuwa ninazungumza kuhusu vinyongo. Ndipo mwanaume huyo kwa namna fulani akachukizwa nalo, nilipolisema. Na nilimwambia miaka kadhaa iliyopita, nilipokutana naye kwa mara ya kwanza, kwamba, "Alisumbuliwa na manung'uniko moyoni mwake." Hakutaka kuamini hilo, nafikiri, mwanzoni, ndipo basi hatimaye daktari akamwambia alikuwa na manung'uniko moyoni mwake. Na asubuhi hiyo alikuwa kidogo amevurugika. Ndipo wakati niliposema hivyo, alichukizwa nalo, na upesi akaanguka akafa, moja kwa moja sakafuni, alianguka sakafuni. Na mke wake akainama chini kumchunguza, na yeye alikuwa ameenda.

8 Basi ilinibidi kunyamazisha wasikilizaji, na kisha kuondoka jukwaani, nikateremka chini mahali alipokuwa, nikachukua mapigo yake ya moyo. Hakukuwa na pigo lolote la moyo. Na macho yake . . . Unajua, moyo ukisita, macho hurudi nyuma upesi. Na nikajaribu kuvuta macho yake, nikamwona katika hali hiyo, na kujua alikuwa ameenda. Ndipo Bwana Yesu akasema, "Nena."

Na mimi nikasema, "Bwana Yesu, mrudishie uhai wake."

Alinitazama, kasema, "Ndugu Branham."

9 Na yeye yuko hai, usiku wa leo, na labda atahudhuria mkutano huu. Amekuwa akiihudhuria muda wote. Na atahudhuria, labda. Simwoni hapa usiku wa leo. Bw. Way, upo hapa? Si—sininii . . . Mbona, ameketi papa hapa mbele zangu. Naam, naam, papa hapa mbele zangu. Sikujua hilo. Na sasa yeye huyu hapa usiku wa leo, mwenye afya kabisa. Waweza kusimama tu ili watu waweze kuona kwamba Mungu anaweza kufufua wafu, kutoka kwenye . . .? Na mke wake, mwuguzi mwema Mnorwe. Akimsifu Bwana! [Kusanyiko linashangilia—Mh.]

10 Je! maskini mke wako mpendwa yu pamoja nawe? [Ndugu Way anasema, "La, anamhudumia yule mtu mgonjwa, Ndugu Branham."—Mh.] Ameenda kushughulika kwa ajili ya . . . kumhudumia mgonjwa. Mke wake ni mtu mwenye upendo sana ambaye hujaribu kuwatunza wagonjwa. Hilo liko moyoni mwake. Yeye huuguza, kila mara. Na yeye anahudumia . . . baadhi ya wagonjwa huko nyuma sasa. Na kwa hiyo tunamshukuru sana Bwana.

11 Sasa, mimi, nikiingia, nilimsikia Ndugu Vayle akizungumza kabla tu ya mimi. Na mimi nitajaribu kila usiku kuondoka mapema kabisa, mapema niwezavyo. Na nitakuwa nikiwaombea wagonjwa, na jinsi tu Bwana atakavyoongoza; na kumwomba Mungu ambariki Ndugu Carlson na kundi lote hapa, katika Chicago, wanaokungojea Kuja kwa Bwana.

12 Labda baadaye kidogo katika juma hili, huenda nitawaambia ono nililopata asubuhi ya leo, muda mfupi baada ya mapambazuko, nilipoanza tu kuja hapa juu, kuhusu hili; na labda wakati mwingine nikipata muda kidogo zaidi katika juma, Bwana akipenda.

13 Sasa, ni wangapi waliopo hapa ambao hawajawahi kuwa katika mmoja wa mikutano hapo kabla, hebu tuone mikono yenu, ambao hawajawahi kuwa katika mmoja wa mikutano. Vema, vema, tuna furaha kuwa nanyi hapa katika maskani hii ndogo, usiku wa leo, na katika ulingo huu, ambapo nafikiri wakati mmoja ulitumiwa kwa ajili ya mwereka (sivyo?) au masumbwi, na kadhalika.

14 Ninakumbuka nilihubiri hapa, si muda mrefu uliopita, huko Vincennes, Indiana . . . Evansville, Indiana, hasa, ambapo niliingia kwenye Golden Gloves, kama m—mtoto. Ndipo nikapata kupigana katika mapigano ya kulipwa, kama mvulana, na nilishinda mashindano kumi na tano ya kulipwa mfululizo. Na nikapoteza moja, na hilo lilikuwa ni kwa sare huko Evansville, Indiana. Na katika ulingo uo huo, ambapo nilikuwa nimepigana na mtu huyu, nilirudi nikihubiri Injili. Nikasema, "Sasa ninapiga vita, si ndugu yangu, bali ibilisi ambaye amekuwa akimfunga ndugu yangu." Hiyo ni . . .

15 Na kwa hiyo tupo hapa usiku wa leo, na mahali hapa pamegeuzwa kutoka kujaribu kufungana mmoja na mwenzake kwa vifungo vya mwereka, na kujaribu kufunga ibilisi katika kifungo kama hicho, kwa Maandiko, hata hawezi kuondoka kwacho mpaka achukue hesabu. Hiyo ni kweli. Na sasa tunaomba kwamba Bwana atatusaidia kufanya hili.

16 Mara nyingine tu sasa, huenda kuna yeyote, kabla tu hatujalisoma Neno, angetaka kukumbukwa katika maombi? Inua tu mkono wako. Ninajua kuna joto humu ndani usiku wa leo, hiyo ndiyo sababu tutaharakisha.

17 Pia, kumbuka, rudi kesho usiku. Na hiyo ni Jumatano usiku, Alhamisi usiku, Ijumaa usiku. Tena nafikiri, Jumamosi asubuhi, niliiona kwenye orodha, kwa ajili ya kiamshakinywa cha Wafanyabiashara, Jumamosi asubuhi. Jumamosi usiku, katika Lane Tech High School. Halafu Jumapili, Jumapili alasiri na Jumapili usiku, hapa. Hebu tuninii . . .

18 Nini? [Ndugu fulani anasema, "Kwa namna fulani zungumza zaidi katika maikrofoni *hii*."—Mh.] Katika hii? Vema. ["Hii papa hapa."] Naam. Mnaweza kusikia hiyo vizuri zaidi? [Kusanyiko

linasema, "Ndiyo."] Ni hiyo? Hiyo ni sawa. Vema, bwana, nitakumbuka kusimama upande *huu*.

Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu.

19 Sasa, Baba wa Mbinguni, tunapokaribia saa hii, ambapo wanaume na wanawake hawana budi kufanya chaguo, tunatambua kwamba hatutaweza kutoka kwenye jengo hili vile tulivyoingia. Hatuwezi kamwe kuingia katika Nyumba ya Bwana, na kutoka vile vile; tunatoka tukiwa bora au wabaya zaidi. Tujalie, Bwana, kwamba tunaweza kutoka, usiku wa leo, bora kuliko tulivyokuwa tukiingia.

20 Na maneno haya machache, na mafungu haya, Maandiko ambayo nimeandika hapa kwa ajili ya Ujumbe mfupi, usiku wa leo, jalia iwe ni kwa ajili ya heshima ya Kristo. Hebu watu Wake, katika kusikia Hilo, wapokee imani, kwa kuwa kwa kweli tunaamini tunaishi katika saa za mwisho za siku ya mwisho. Jua limekuwa likitua kwa muda mrefu. Uvumilivu wa Mungu umelishikilia. Ni vivuli vinakusanyika sasa. Na sisi tunaomba, Mungu, kwamba Wewe utatujalia tutambue hili zaidi ya tulivyowahi kutambua hapo kabla katika maisha.

21 Wabariki wale watu walioinua mikono yao. Samehe dhambi zetu. Tupe imani katika Neno Lako na Kuja kwa Mwana Wako. Kwa kuwa tunaomba hayo katika Jina Lake na kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

22 [Mtu fulani anasema, "Na waliuliza kama ungeomba. Yupo mama huko nyuma, alikuwa mgonjwa sana, sana, na amezirai."—Mh.] Hebu kidogo. Yupo mama huko nyuma kabisa, ambaye amezirai, ninaamini ndivyo, na yeye ni mgonjwa. Hebu tuombe tu.

23 Baba wa Mbinguni, katika Jina la Yesu Mwana Wako, jalia nguvu zilizomfufua yule kijana usiku ule, aliyeketi usiku kucha, akimsikiliza Paulo akihubiri, jalia nguvu zizo hizo zilizomfufua kuwa mzima tena, naomba zifanye vivyo hivyo kwa huyu dada yetu ambaye amezirai, labda kwa sababu ya joto, na yuko huko nyuma mgonjwa. Jalia Roho Mtakatifu, Bwana, wa Uzima, aje juu yake na autie nguvu uhai wake wa kimwili. Jalia hili, Bwana. Tunalikabidhi Kwako sasa, katika Jina la Yesu Kristo Mwana Wako. Amina.

24 Hebu nisikie kutoka kwako. Ikizidi kuwa mbaya, nitarudi na kumwona.

25 Sasa katika Kitabu cha Yohana Mtakatifu, mlango wa 12 na kifungu cha 32, ningependa kusoma kwa ajili ya sehemu ndogo ya Maandiko, katika njia tu ya kufanya fungu, kujenga muktadha. Na mimi ninaona kuwa ni vigumu kwenu kunisikia, ninaweza kujua jinsi mnavyofanya, mwangwi katika—katika jengo, na nitajaribu kuzungumza wazi tu niwezavyo. Ninataka kusoma fungu hili, Yesu akizungumza:

Na *mimi, nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta* watu *wote kwangu.*

26 Ninataka kuchukua hili kwa ajili ya fungu: *Kuna Njia Moja Tu Iliyotolewa Na Mungu Kwa Kitu Chochote.* Njia moja Mungu ametoa kukabiliana na kila kitu. Sasa, njia nyingine yoyote, kando na njia hii, ingekuwa ni njia iliyopotoshwa, kwa ile ya Mungu. Mungu anaweza kuwa tu na njia moja ya kufanya chochote. Njia Yake ya kwanza daima ndiyo njia pekee ambayo Yeye anaweza kukifanya. Kwa kuwa, Mungu, akifanya chaguo ama uamuzi, lazima adumu daima na uamuzi huo. Na iwapo Yeye atabadilisha uamuzi huo, kwa njia iliyo bora, basi inaonyesha kwamba Mungu si Mungu, Yeye si asiye na kikomo, alipata kitu fulani bora kuliko kile Yeye alichojua hapo mwanzo. Yeye, Yeye habadiliki. Yeye hufanya njia Zake kamilifu. Maneno Yake ni makamilifu. Na njia yoyote ambayo huondoa, au kuongeza kwa, chochote ambacho Mungu ametoa, ni kosa.

27 Ninaamini, katika Kitabu cha mwisho cha Biblia, kiitwacho Ufunuo, imeandikwa, "Mtu awaye yote akiongeza neno moja, au kuondoa Neno kutoka kwa Hilo, yake ile, sehemu yake itaondolewa kutoka kwenye Kitabu cha Uzima."

28 Na sasa, kwa hiyo, Mungu amefanya njia, na njia kamilifu, na hatuna budi kutembea sawa na hiyo, si kujaribu kufanya Hilo kuwa bora, si kujaribu kuondoa chochote kutoka kwa Hilo, kuingiza chochote, au kuondoa chochote kwa Hilo. Hatuna budi kuchukua Hilo vile tu Mungu alivyoliweka Hilo. Chochote kingine ni uwongo.

29 Hata katika Kitabu cha Mwanzo, mwanzo, Mungu alisema, katika Mwanzo 1, akizungumza kuhusu maumbile. Alisema, "Kila mbegu na izae ya aina yake." Kila mbegu lazima idumu kwa aina yake. Sasa, kubadilisha hilo, kungekuwa ni kufanya jambo ambalo Mungu alisema lisifanywe.

30 Na sasa tunaona, na sasa hebu mwangalie mwanadamu, kile ambacho amefanya kwa kuchanganya njia ya Mungu ya uhai. Tunataka kuchukua hili kwa ajili ya msingi, kusema kile ninachotaka kuwaambia kumhusu Bwana Yesu. Unaona, wakati mwanadamu . . . Wakati Mungu alipoifanya mbegu, Yeye aliifanya kamilifu, na sasa mwanadamu amejaribu kuingiza kitu fulani katika hiyo mbegu.

31 Kwa mfano, leo, nikija huku, niliona huko Indiana ya kusini, na kote kupitia Indiana, na kuendelea, kulikuwa na, kile tulichosema, "mhindi chotara." Na jinsi mhindi huo ulivyo suke kubwa la kupendeza, bali haufai kitu. Huonekana bora, lakini si bora. Haufai kabisa.

32 Basi tunakuta, kwamba kwa kuzalisha kuku kichotara, tunakuta kwamba . . . Je! mliwahi kujaribu kula kuku aliyekaangwa siku hizi? Vema, ni vigumu kumla. Hu—hunukia na ana ladha tu kama, ninamaanisha, ana ladha kama kuku

alivyonukia. Kwa hiyo ni kitu gani? Kuna watu mia nane wamelazwa wagonjwa katika Jeffersonville, Louisville na New Albany, sasa, kutokana na kula mayai kutoka kwa kuku chotara. Unaona, wamechukua kuku na kumzalisha njia mbalimbali.

33 Na halafu, jambo jingine, wanafikia mahali ambapo wananyunyiza kwa kutumia kitu hiki cha mbu, na kupata hii DDT. Kuku na wanyama wanachukua hiyo.

34 Sisi kwa hakika tunaishi katika siku ya mwisho. Wanazalisha vitu mbalimbali pamoja, wakichanganya, na inafanya bi—bi—bidhaa isiyo nzuri.

35 Kupitia kufanya hivi, nilikuwa nikisoma kwenye jarida la matibabu, naamini lilikuwa, na halafu katika *Reader's Digest,* kuhusu jinsi ambavyo imebadilisha mkondo wa maisha ya watu. Hata inawapotosha wanaume na wanawake, hata wanaume wanakuwa zaidi kama wanawake, na wanawake kama wanaume. Wanaume wanakuwa do—dondoadume, na—na wanawake wanakuwa wa kiume. Ni vitu vilivyochanganywa. Unaona, seli hiyo ambayo tunakula kutoka kwa mnyama huyu ambaye ni chotara, kwa kweli si seli ifaayo kwetu sisi. Hivyo basi, katika kufanya hivyo, unaona, seli hiyo kutoka kwa mnyama huyo, ama seli kutoka kwa ngano, au kutoka kwa mhindi, si seli ifaayo.

36 Ili kufanya hii ikue, ionekane kuwa kubwa zaidi, haina budi kunyunyiziwa kila wakati.

37 Sasa, mmea halisi, mmea mzuri wenye afya, hauna haja kunyunyiziwa hata kidogo. Hakuna wadudu watakaousumbua, kwa sababu una kifukuza wadudu, wenyewe, ambacho huo unatoa, ambacho huwafukuza wadudu wote kutoka kwake. Sasa, hiyo ni njia ya Mungu.

38 Kilicholeta ugonjwa ulimwenguni kilikuwa ni dhambi. Wakati mwanadamu alipoanguka kutoka kwa njia ya Mungu iliyotolewa, alijiweka wazi kwa kila pepo aliyekuwepo, kwa ugonjwa, na kadhalika. Kwa sababu, inambidi kuweka dawa, na kunyunyiziwa, na ni kila kizazi kuzalishwa katika kingine. Sasa huenda ukawa ni Mkristo, na mke wako huenda akawa ni Mkristo; lakini jeni za mwili wako zingali ni urithi kutoka kwa baba yako na babu yako, na kote chini. Kama Danieli alivyosema, "Kila kizazi kitakuwa dhaifu zaidi na werevu zaidi." Na imefanya jamii nzima, jamii nzima ya wanadamu, kufa.

39 Wazia tu, miaka michache iliyopita, hukuwahi kusikia kuhusu yeyote kuumia akicheza besiboli. Sasa inawabidi kutumia kofia za chuma, kupiga nazo mpira kwa kutumia gongo, wanaua wengi sana kila mwaka. Ukimgonga mtu, yeye ni mnyonge sana, ni kama nungubandia, anakufa tu sasa hivi. Na unaona, tena, walikuwa . . .

40 Kama hii masumbwi, ninaamini ilikuwa Bob Fitzsimmons na Corbett, walipigana raundi mia moja ishirini na tano. Sasa

raundi mbili hadi kumi, na halafu inakubidi kuwafanyia kazi kwa mwezi mmoja kuwarudisha katika uhai tena. Na wakati ule walipigana mikono mitupu, na sasa tuna tandiko la manyoya kuzunguka mi—mikono yetu wakati tunapopigana. Na sasa wanaenda kulazimika kukomesha mchezo huo, ni kwa sababu kila mara ukimgonga moja, karibu inamwua. Unaona? Na unaona, wewe, ni . . .

41 Na jamii yote imekwisha. Hakuna tumaini lolote lililosalia. Kila kitu kiko katika mwisho wake: ng'ombe, mahindi, kila kitu.

42 Sasa, huwezi kuchukua mmea ambao umepandwa, na kuuchanganyisha katika kitu fulani, kuurudisha tena na kuupanda, hautafaulu. Hautajizalisha wenyewe. Hauwezi. Kwa sababu, Amri ya Mungu ingali inasimama vile vile, "Kila mbegu lazima izae ya aina yake." Kama sivyo, ni mbegu chotara ikiwa na uhai uliopotoshwa, na hivi punde itakufa. Ukipanda mhindi chotara, utakua kufikia karibu ambapo suke linapaswa kuingia, utageuka manjano na kujikunja.

43 Sasa hivyo ndivyo ambavyo wamefanya kupitia wanyama. Wamefanya hivyo kupitia mbegu. Wamefanya hivyo kupitia kila kitu kingine.

44 Pia wamefanya hivyo kanisani. Imejaribu kuunda kanisa linalopendeza zaidi, mahali bora, ki—kitu cha kupendeza, vitu vikubwa. Wamelichanganya, kwa kulichanganya na namna fulani ya mafundisho ya kujibunia ya mwanadamu, na kadhalika, nalo huja kufikia kwenye Neno, ambapo Hilo lingeweza kujizalisha tena, na kufa tena. Unaona? Na kuna . . . Wewe kwa urahisi tu . . .

45 Kuna njia moja ya kufanya chochote, na hiyo ni njia ya Mungu. Na nje ya hiyo, yote yako nje, kwa sababu hakitajizalisha chenyewe tena. Ninayo Maandiko kwa ajili ya mambo haya, kuthibitisha kwamba inapaswa kuwa hapa katika siku za mwisho.

46 Niliposikia hali hiyo ya yai hivi majuzi, nilirudi katika kitabu changu ambapo Bwana alinena nami katika 1931, na hapo nilikuwa nimeandika katika kitabu changu, "Katika siku za mwisho, waonye watu wasile mayai wala kuishi katika bonde." Na, unaona, sijui kile kuanguka na mambo yatakachokuwa, unaona, bali hata hivyo Bwana alionya hilo kimbele, huko nyuma miaka thelathini iliyopita, unaona, "Kutoishi katika bonde, katika siku za mwisho," na, "Msile mayai," kila kitu kitatiwa sumu. Unaona? Na hilo ndilo hasa lililotendeka. Sasa wazia hilo, miaka thelathini na kitu iliyopita.

47 Neno la Mungu ni mbegu. Yesu alisema hivyo, kwamba, "Neno la Mungu lilikuwa ni Mbegu ambayo mpanzi alipanda." Na *Hii* ndiyo Mbegu pekee ambayo itazalisha Uzima wa Milele. Sasa tunaweza kuwa na namna zingine zote za maisha, bali maisha . . . maisha ya kanisa, maisha ya nyumbani, maisha ya

familia, maisha ya taifa. Bali Uzima wa Milele pekee huja kupitia Neno la Mungu. Hilo ndilo—hilo ndilo Mbegu pekee inayoweza kuzalisha Uzima wa Milele. Na sasa wanajaribu kufanya, wanachanganyisha *Hili* na kanuni ya imani, kuweka kanuni fulani ya imani, kibandiko fulani cha kimadhehebu au kitu fulani katika Hilo. Na kile ambacho wamefanya, kwa kufanya hili, kimefikisha kanisa mahali hata linakua kufikia mahali ambapo linapaswa kuwa likipokea Mbegu, Neno halisi, na ni hali ya mchanganyiko, litaanguka na kurudi kwenye fundisho lake la kimadhehebu, na kuliacha Neno halisi la Mungu.

48 Hivyo basi, tuko kwenye wakati wa mwisho. Hakuna tumaini hata moja lililosalia. Hatuwezi kujenga juu ya taifa hili. Taifa hili limejengwa juu ya siasa. Siasa zimekwisha. Wao ni... Imeoza tu kadiri iwezavyo kuwa. Wakati wewe...

49 Je! mlisoma jarida la *Life*, ambapo huyu wakili, ama—ama huyu hakimu, mwanawe, mvulana? Alikuwa mkali sana katika kushindana na hawa kina Riki, na kadhalika, hapa nje, magari haya yenye mbio kuliko yote. Na mvulana wake akaua kundi la watu, mvu—mvulana mdogo, maskini mtoto mvulana, na kundi. Naye hakimu akamwacha huru. Yote mchezo wa siasa!

50 Unaona, maisha ya kitaifa yamekwisha. Uhai wa kawaida wa mimea umekwisha. Umechanganyishwa sana na kila kitu mpaka hauna uhai ndani yake. Maisha ya mwanadamu ni mchafuko kila mara.

51 Na maisha ya kiroho yako katika kiwango cha chini kabisa yalivyowahi kuwa. Unaona? Unaona, hapo, yamechanganywa sana. Kila kitu kilizalishwa ndani yake na kuongeza kitu ndani yake, kuyafanya bora kwa njia *hii*. Nawaambieni, hata kwa huduma zetu za Kipentekoste; wakati, tulizoea kwenda huko chini katika maskini baa namna hii, na mahali.

52 Niliongoka katika baa iliyogeuzwa. Na mimi ninajisikia nyumbani sana sasa. Ninatazama nyuma pale na kuona ile kaunta, na kadhalika. Lilikuwa ni maskini, kanisa la watu weusi, ambapo nilipokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, niliongozwa huko na Bwana.

53 Sasa, kuona mahali pa namna hii, hao—hao hawataki kuona. Inawabidi kuwa na jina kubwa lenye sifa nyuma yake. Hapana budi pawe na mengi sana nyuma yake, la sivyo watu hawataninii...Lazima pawe panapopendeza sana, kwa nje, mpaka ikiwa si—sivyo palivyo, basi watu hawataki chochote kuhusiana napo.

54 Lakini tazama Neno la Bwana! Sasa, Mungu anayo njia ya kufanya mambo, na sisi hatuna budi kulifanya kwa njia ile Yeye anataka lifanywe. Kama sivyo, basi haina nguvu. Yesu alipata kitu kama hiyo, wakati Yeye alipokuja katika siku Yake. Alisema, "Nyinyi, kwa mapokeo yenu, mmelitangua

Ne—Neno la Mungu, kwa mapokeo yenu.” Unaona, walikuwa wamechanganya ndani yake, wakaingiza katika Amri za Mungu mapokeo yao wenyewe, ambayo yalizitangua Amri.

55 Leo hii, ninajua limekuwa ni jambo lile lile. Hakuna kitu kilichosalia, rafiki yangu Mkristo, ila Kuja kwa Bwana Yesu Kristo. Hilo ndilo tumaini pekee kanisa lililo nalo. Kadiri linavyokuja, kama likiwahi kuchukua dhehebu tena, limekwisha, kwa sababu kila dhehebu limekwisha linapofanyika dhehebu. Ni jambo lile lile . . .

56 Nitasema jambo fulani hapa, mimi labda sipaswi kusema, bali hata hivyo ninaamini inanipasa kulisema.

57 Kama ulitambua, Lusifa anafanya jambo lile lile hasa, leo hii, ambalo alifanya pale mwanzo. Unaona? Lusifa, pale mwanzo, alitaka kujijengea ufalme ambao ulikuwa mkubwa na wa kupendeza zaidi ya ufalme wa Mikaeli, Kristo. Yeye, hizo zilikuwa ndizo shauku zake, kutimiza jambo kama hilo. Na alipata kulifanya kwa kitu gani? Alichukua malaika walioanguka ambao walikuwa wameacha makao yao ya kwanza. Alichukua hao ili kuwatumia kulitimiza.

58 Tena, leo hii, Lusifa ameingia ndani ya kanisa, na kuondolea mbali Neno, na kuingiza dhehebu. Na yeye anajenga kanisa, tapo la ekumeni linaloendelea sasa, kuunganisha waprotestanti wote pamoja, na wote pamoja waingie katika Katoliki. Na huyu papa waliyemwingiza sasa, kufanya jambo lile lile, hasa kile Maandiko yaliyosema lingefanya. Na yeye anafanya hilo kwa kitu gani? Anafanya hilo kwa watu wa hayo matapo makubwa ya ekumeni, ambao hawamjui Mungu; na wengi wao katika Pentekoste, maana wanafanya jambo lile lile. Ni kitu gani? Yeye anafanya hilo na malaika walioanguka, Walutheri walioanguka, Wamethodisti walioanguka, Wapentekoste walioanguka, walioacha makao yao ya asili kutoka kwenye Neno la Mungu, na kurudi moja kwa moja ndani kuunda tapo kubwa la ekumeni. Wajumbe walioanguka, wajumbe ambao wakati mmoja walikaa na Neno, bali wakauza haki zao za mzaliwa wa kwanza na kujiunga na ulimwengu. Jambo lile lile, liko kwenye siku ya mwisho. Na Lu- wao . . . Na Lusifa anatimiza leo hii, kwa njia ya watu wenye roho hizo ndani yao, alilofanya na malaika pale mwanzo, malaika walioanguka ambao hawakulinda makao yao ya kwanza kumtii Mungu. Na yeye anafanya jambo lilo hilo leo hii.

59 Loo, kamwe hutapata njia yoyote, njia yoyote hata kidogo; sijali kama uko kwenye baa, ama uko mtaani, au popote ulipo. Njia ya Mungu iliyotolewa kwa mwanadamu, kuja kwa Kristo na kupokea Uzima wa Milele. Yesu alisema, “Mimi, kama nikiinuliwa juu kutoka duniani, nitawavuta watu wote Kwangu.” Hiyo ndiyo njia ya Mungu ya pekee.

"Kama nikiinuliwa juu kutoka duniani, nitawavuta watu wote Kwangu."

60 Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Alisema, katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 14 na kifungu cha 12, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo yeye atazifanya pia." Njia ya Mungu iliyotolewa. Marko 16 ilisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Katika Jina Langu watatoa pepo. Watanena kwa lugha mpya. Kama wakishika nyoka au kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru. Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Mambo yale yale aliyofanya Kristo! Hiyo ni . . .

61 Yeye alikuwa ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Yeye alikuwa ni ahadi ya Mungu, ikithibitishwa. Yeye alikuwa—Yeye alikuwa ni Mungu katika umbo la mwili. Biblia ilisema kwamba, "Mungu alikuwa ndani ya Kristo." Yule Yehova mkuu aliyeumba mbingu na nchi, alidhihirishwa katika mwili, Bwana Yesu. Na ndani ya huyo Mtu mmoja, Yeye aliweza kutimiza. Mpaka . . . Alijaribu hilo kupitia Musa, na Yeye alilijaribu katika Yakobo, na yeye alilifanya katika Yusufu. Bali Yeye alikuja katika utimilifu Wake, ndani ya Mwanadamu Kristo, Yeye alikuwa ndiye utimilifu wa Mungu kwa jinsi ya mwili, ambapo Mungu aliweza kujidhihirisha Mwenyewe. Ndipo Yeye akasema, "Ni nani awezaye kunihukumu Mimi kuwa nina dhambi? *Dhambi* ni 'kutokuamini.' Ikiwa sijafanya hasa kile Maandiko yalichosema nitafanya, basi ni nani awezaye kunihukumu Mimi na kusema mahali ambapo nilishindwa kwa njia moja?" Unaona, ni njia ya Mungu iliyotolewa.

62 Ndipo Kristo, Yule Mwenye haki, ilibidi afe ili kwamba alete Uzima wa Milele kwa Damu Yake, kutoa seli Yake ya Damu, kwamba Yeye aweze kutupatia Uzima wa Milele. Hiyo ni njia ya Mungu iliyotolewa.

63 Kamwe hakujawahi kuwa na chochote kilichoshinda njia ya Mungu kwa chochote. Sijali ni kitu gani. Kama watu hawatajaribu kuingiza mawazo yao wenyewe, bali walichukue tu jinsi Mungu alivyolisema, kuliamini Hilo. Unaona, inaonekana kuwa ni vigumu sana kwa mwanadamu kuondokea tu mawazo yake mwenyewe, ni kwamba tu lazima awe na kitu cha kufanya katika Hilo, mwenyewe. Yeye daima amechafua, kama mtasamehe tamko hilo, yeye daima amechafua njia ya Mungu kwake, kwa kuingiza njia yake mwenyewe katika Hiyo.

64 Je! wamewahi, unafikiri wangeweza kupata njia bora kwa kifaranga kuzaliwa, kuliko kudonoa njia yake kutoka kwenye ganda? Sijui kama ungeweza kupata njia yoyote bora. La, bwana. Amezaliwa na maskini kitu cha kutobolea mwishoni mwa mdomo wake mdogo. Na kila mara kichwa chake kidogo kinapoitika kwa kuenda mbele na nyuma, "Amina, Amina, Amina," anakwaruza ganda hilo mpaka anakwaruza na kutoka

nje. Naam, bwana. Kamwe hutapata njia iliyo bora, kwa sababu hiyo ndiyo njia ya Mungu iliyotolewa.

65 Sasa, vipi kama alikuwa na hicho kitu cha kutobolea kwenye mdomo wake, na wewe ulisema, "Maskini kifaranga mdogo; unajua, ninaenda kukupatia njia iliyo bora, ninaenda tu kupasua ganda hili na kukutoa kwa mkono"? Ingemwua. Hiyo ni kweli. Angekufa. Asingeweza kuishi.

66 Inambidi kufanya hivyo ili aweze kujenga nguvu zake za kutosha kupokea hewa na kadhalika wakati akitoka nje. Kama yeye. . . Amepewa kifaa. Anacho hicho kitu kidogo cha kutobolea. Mmekiona, ndege wadogo na kuku. Na wakati anapopiga maskini kichwa chake, anakwaruza hilo yai huku na huku mpaka anapenyeza njia yake na kutoka nje.

67 Kama utachukua hiyo kama mfano, ama katika njia ya kutoa hoja, hiyo ndiyo njia ya Mungu kwa ajili ya Wakristo kuzaliwa. Si kutembea kuja madhabahuni na kumpa mtu fulani mkono wako wa kulia, na kuweka jina lako kwenye kitabu. Bali kuenda huko chini na kuchungulia na kulia na kusihi na kuomba mpaka Mungu akupe nguvu, ndipo unatoka kwenye ganda la ulimwengu.

68 Ikiwa mtu fulani, mchungaji, atapasua tu ganda na kukutoa, aseme, "Loo, vema, hilo ni sawa, tutakuingiza ndani kwa vyovyote vile," umekufa. Ni hayo tu kwa hilo.

69 Huna budi kuja kwa njia ya Mungu iliyotolewa. Na hivyo ndivyo ilibidi wale wengine kuja, kwa kuzaliwa kwa Roho wa Mungu. Kaa hapo mpaka! Muda gani? Mpaka! Aliyaambia makundi ya kwanza ya wapentekoste "kungojea katika mji wa Yerusalemu, mpaka." Haileti tofauti yoyote, siku moja, siku tano, siku tisa, au chochote kilichokuwa, kaa hapo mpaka wamejazwa na Roho, mpaka wazaliwe tena.

70 Mabata na mabata bukini, hawajawahi kupata njia kwa ajili ya mabata na mabata bukini ku—kujiandaa kuja Kusini, kutoka Kaskazini hapa, kuliko njia ya Mungu iliyotolewa kwa ajili yao kukusanyika. Wakati fulani uliopita, nilikuwa na somo kubwa juu ya hilo. Nilikuwa chini huko Texas, na nikaona, tulikuwa tunateremka barabarani, na magari yalisimamishwa kwa karibu nusu maili. Ndipo nikaambia baadhi yao, "Shida ni nini?"

Akasema, "Mabata bukini wako kote barabarani."

71 Vema, hatimaye, nilipofika huko juu, usingeweza kujisikia mwenyewe ukiwaza. Walikuwa na uamsho. Wote walikuwa wanajitayarisha kwa ajili ya kuruka. Walikuwa wanaenda nyumbani, wakienda juu Kaskazini kwa nyumba yao, ambapo wangeweza kuwakuza wengine wadogo. Na walikuwa na uamsho, wakikusanyika, kabla ya kuenda.

72 Sasa, hiyo ni njia ya Mungu iliyotolewa, kukusanyika, wote wanajumuika pamoja. Mmoja alikuwa *hapa*, na mwingine *pale*,

na mwingine huko mahali pengine, mmoja katika shamba moja la mpunga, na mmoja katika shamba la ngano; lakini kitu kingine, kwa njia fulani, katika siku fulani, (sijui ni kwa nini, kwa njia gani), lakini katika siku fulani, hapa wote wanakuja pamoja, ilionekana kama kitu fulani kiliwavuta. Tunakiita "silika." Ni silika iliyotolewa na Mungu, kukutanika pamoja kabla ya kuruka.

73 Unaona kile Mungu anachojaribu kufanya sasa? Kuvuta Kanisa Lake kutoka upande mmoja hadi mwingine, kupata uamsho, uamsho wa mtindo wa kale kama mabata bukini wamefanya daima.

74 Sasa vipi kama walijaribu njia nyingine, kasema, "Vema, sasa tutaichukua tu njia nyingine"? Kamwe wasingefika huko. La, bwana. Vipi kama ungesema, "Vema, sasa nitakwambia nini, tutafanya njia iliyo bora kwa ajili yao. Tutawakusanya wote kwenye kizimba na kuwapeleka juu kwenye kizimba, tuwaweke katika kizimba kidogo cha kuku, au kukitengeneza kizimba cha bata au kizimba cha bata bukini, au chochote unachotaka kukifanya, na kuwaweka ndani ya hicho na kisha tuwapeleke huko juu"? Unafikiri hiyo ingekuwa ni njia bora, useme, "Loo, tunaweza kuwapatia . . . Loo, nakwambia, tungeweza kuwalisha vyema zaidi, barabarani"? La, huwezi.

75 Kuna nafaka ambayo iko katika vidimbwi na makondeni, magugu na kadhalika ambayo inawabidi kupata, ili kuwapa nguvu kuwa kile walicho wakifika kule. Wao, kama hawakupata hiyo, wasingekuwa . . . wasingeweza kukuza watoto wao. Wasingekuwa mabata halisi. Wangekuwa waliochanganywa mbegu kama tulivyo, unaona, kama ingewabidi kuchukua hiyo. Lakini Mungu ana njia ya—ya kufanya hilo.

76 Uwaweke katika kizimba, unajua kile mabata hao wangejua sasa hivi? Waweke katika dhehebu namna hiyo, walijua kwamba walikuwa tayari kwa kichinjio. Hayo tu. Hilo ndilo unalofanya ukiwaweka pamoja katika kizimba, wanaenda kwa ajili ya kuchinjwa. Mabata wana ufahamu bora kuliko tulio nao, katika hilo. Ukienda kuwaweka wote katika kizimba katika gereza lililobuniwa na mwanadamu, vema, basi, unaona, bata anajua hana uhuru wake kuruka hewani, na kufanya kama Mungu alivyompa kufanya. Na kumweka katika kizimba, basi yeye—yeye amekwisha. Hivyo tu. Unawatia katika kizimba wakati wanapowachinja. Naye bata anajua vizuri zaidi. Tunapaswa kujua.

77 Wala huwezi kuwachagulia njia bora ya kuenda. Njia, ukitaka kuiita, hapa juu, nafikiri. Chini nyumbani, huko Kusini, ingali ni *njia*, lakini hapa juu nafikiri wanaiita njia. Unafikiri, kama ungesema, "Sasa sikilizeni, nitawaambieni kile mnachopaswa kufanya. Mnapaswa kurudi kwa njia fulani na kuteremka njia nyingine, halafu chini upande huu." Je! unafikiri

ungeweza kuwachagulia njia bora kwao kuenda, kuliko njia ya Mungu iliyotolewa kwao kuenda? Vema, ungewaingiza katika namna fulani ya ki—kitu, ungewavuta kupitia hapa kwa namna fulani ya sumaku au kitu fulani. Kamwe wasingeninii . . . Ungewavuta kupitia dhoruba, na kupitia kila kitu kingine, nusu yao wangepotea.

78 Vema, huwezi kuwapatia njia bora. Wao, wao huenda njia ya Mungu iliyotolewa. Wanaweza kunusa dhoruba hizo, maili nyingi huko mbali, na kujua jinsi ya kujiweka chini na kuwa tayari kwa ajili ya hizo dhoruba, na kuinuka tena. Mungu anayo njia iliyotolewa kwa ajili yao, nao wana hisi ya bata ya kutosha kuifuata njia ya Mungu iliyotolewa. Sisi hatuna. Tunajaribu kufanya njia bora kuliko ile Mungu aliyotufanyia. Unaona, tunataka kuwa na kitu ndani yake, sisi wenyewe. Bata hazingatii ni nini; yeye huenda tu vile Mungu anavyomtaka aende, jinsi babu zake walivyofanya, jinsi nyanya wa nyanya wa nyanya wa nyanya wa nyanya wa mama yake alivyofanya, na kuendelea namna hiyo.

79 Ikiwa tungechukua tu ukoo wetu kurudi nyuma, hadi Pentekoste, tungejua jinsi ya kufika kule. Mungu alikuwa na njia iliyotolewa, kwa Neno Lake na kwa Roho Wake Mtakatifu. Lakini sisi tunataka kuenda njia nyingine ambayo Daktari *Nanii* alisema, au kundi fulani la watu walikutanika pamoja na kusema. Hiyo ni mbali na njia ya Mungu iliyotolewa. Kanisa lilisafiri vyema katika njia ya Mungu iliyotolewa, hadi kwenye baraza kule Nikea, Rumi, na huko ndiko walikofanyia kosa lao baya. Vipi kama uliweza kuchukua . . .

80 Na sasa unawazia kuhusu kuwatafutia njia iliyo bora, ama je! unaweza kuwatafutia kiongozi aliye bora kuliko kiongozi wa Mungu aliyetolewa kwa ajili yao? Sasa labda ungeweza kuchukua maskini bata dume hapa nje mahali fulani, na kumpeleka huko nje na kumlisha vitamini fulani, na kadhalika, na kumpa wito maalum, wajua. Umtume huko nje, na kutia honi ndogo kinywani mwake, kusudi uweze kuwa na m—m—mdundo ambao karibu angeweza kuimba kwa madoido na hiyo, na huenda ukaliandika katika magazeti yote, "Ba—bata anayeweza kuimba kwa madoido. Na, loo, mabata wote hawana budi kumtafuta. Yeye atajua ni njia gani ya kuwapeleka, kwa sababu yeye kwa kweli amestaarabika na kuelimishwa, na amejipamba. Anaweza kufanya hilo." Wewe huenda . . . Huenda akaketi huko nje na kuimba kwa madoido, alasiri yote, hakutakuwa na bata atakayekuja karibu naye.

81 "Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu, mgeni hawatamfuata."

82 Huenda akasikika wa kupendeza zaidi. Huenda akawa na mabawa yaliyo bora. Yeye—yeye huenda amelishwa vizuri zaidi. Huenda akawa ni bata aliyestaarabika zaidi. Huenda akaweza

kujisokota au chochote, huko nje. Usingeweza kujua kile angeweza kufanya. Bali ninakwambia, mabata wasingemfuata kama hakutoa ile sauti fulani iliyo sahihi. Hiyo ni kweli. Mabata wanajua kiongozi wao, kwa sauti iliyotolewa na Mungu, silika iliyotolewa na Mungu. Na kamwe hutaweza kumpata mmoja aliye bora kwa vyovyote kuliko huyo, maana hiyo ndiyo njia hasa ya Mungu iliyotolewa kwao.

83 Basi tazama, tena, kama ulikuwa umemfunza maskini bata bukini ama bata, kuchukua kundi hilo, wewe labda ungemchukua moja kwa moja katika msongamano wa bunduki ya marisau, ambapo watu wanamtazamia. Lakini, unajua, huyu kiongozi aliyetolewa na Mungu humpeleka mahali palipotolewa na Mungu alipo napo kwa ajili yake. Humpeleka moja kwa moja, mbona, huko Louisiana, na chini katika mashamba ya mpunga ambapo wanalindwa, mwaka mzima. Mbona, hakika. Mungu anajua la kufanya, naye bata anajua kufanya kile Mungu anachomtaka afanye, au alichotoa kwa ajili yake. Angalia.

84 Je! ungeweza kufikiri ungeweza kubuni chombo bora kilichotolewa kuliko kile Mungu alicho nacho kwa ajili yake? Sasa, maskini bata huyo hakuondoka kwenye kidimbwi. Alizaliwa huko katika misitu ya kaskazini. Hakuwahi kamwe kuondoka kwenye kidimbwi, maishani mwake, lakini kwa njia fulani yeye anaogelea moja kwa moja kuelekea juu. Anaweza kuenda mashariki, magharibi, kaskazini, kusini, njia yoyote atakayo kuenda; bali kitu fulani kinamshurutisha kuenda moja kwa moja kusini, humwambia jinsi ya kupita vipindi vya baridi, dhoruba na kila kitu, na kuondoka katika hayo, moja kwa moja mahali chakula kilipo. Mungu anacho chombo ndani ya huyo bata, kinachomwongoza tu sahihi hasa. Na hawajawahi kamwe kuweza kupata njia yoyote bora kwa ajili yake (la, bwana) kuliko njia ya Mungu iliyotolewa.

85 Wao, wao hawajaweza kamwe kupata njia bora kwa mtoto kupata kile anachotaka, kuliko kukililia. Wewe huenda, huenda ukamwambia, "Vema, angeweza—angeweza kutikisa ngumi yake ndogo, ama angeweza kupayuka namna hiyo," bali kamwe hatapata kuvuta usikivu kama kulia. Hana budi kukililia. Hivyo tu. Huenda ukasema, "Vema, sasa, nitaiwasha saa yangu ya kengele. Na inanibidi kumlisha mtoto huyu kwenye wakati maalum, dakika fulani, hadi dakika fulani, muda mwingi nilio nao kumlisha." Unaiwasha saa hiyo ya kengele, na kutia chupa kinywani mwake, atapayuka na kuitema nje. Yatie maziwa kinywani mwake, na yeye atayatema nje. Si wakati bado. Lakini Mungu anayo njia iliyotolewa, Yeye huiwasha saa hiyo ndogo ya kengele, *hapo* chini, na, ikiwa hivyo, hatakoma mpaka aipate chupa yake. Hivyo tu. Anaililia.

86 Sasa, Mungu hupendekeza njia hii, pia, kwa watoto Wake wachanga, kulia, waaminio Wake kulilia kile wanachotaka. Hiyo ni kweli. Mlilie Yeye, kwa ajili ya haja zako.

87 Sasa, usisikilize hotuba za kielimu, mtu fulani anasema, "Vema, sasa nakwambia, huu ubatizo wa Roho Mtakatifu wanaozungumzia, huu uponyaji wa Kiungu, na vitu vya namna hiyo, vema, nakwambia, si kwa ajili ya . . . sivyo, leo hii; ninaweza kueleza hilo, kwamba si kwa ajili ya leo hii." Sikiza, mtoto halisi wa kweli wa Mungu hatasikiliza hayo.

88 Atalia kwa nguvu, na kupiga mayowe, na kuchapua miguu yake, mpaka apate jibu lililothibitishwa likirudi kutoka kwa ahadi hiyo kutoka kwenye Neno la Mungu, maana, "Mtu haishi kwa mkate pekee, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu, litokalo katika kinywa cha Mungu." Yeye hulia na kulia mpaka Neno hilo la ahadi linapothibitishwa. Mtoto mdogo wa Mungu akiishi juu ya Neno la Mungu, hakuna njia iliyo bora ulimwenguni kwa ajili yake. Ni hayo tu. Yeye anaishi juu ya kile Bwana anachosema kwa ajili yake kuishi kwacho, na anakaa hapo mpaka litendeke; analia, anachapua miguu yake, na hubakia tu kwenye hilo.

89 Baadhi yao wanasema, "Loo, huwezi kupokea Roho Mtakatifu, hakuna kitu kama hicho." Walijaribu kutuambia kwamba miaka iliyopita, kwamba hakukuwa na kitu kama kunena kwa lugha, na unabii, na karama hizi zote kuu ambazo Mungu aliahidi katika kanisa la mwanzoni, na kuwapa. "Siku hizo zimepita."

90 Unafikiri hilo liliwakomesha hao watu wenye njaa moyoni? Walilichukua Neno hili, na wakajua kwamba Biblia ilisema Yeye . . . "Ahadi ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, hata wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu." Walikaa hapo juu ya nyuso zao, wakalia, na kuomba, na kuchapua miguu yao, na kupiga mayowe mpaka Mungu akamwaga Roho Mtakatifu yule yule, juu yao, ambaye Yeye alimwaga juu yao hapo mwanzo. Amina. Ni kitu gani? Ni njia ya Mungu iliyotolewa. Hiyo ni kweli. Waliiamini, na Mungu akatoa njia kwa ajili yao. Petro aliwapatia njia iliyotolewa kwenye Siku ya Pentekoste.

91 Baadhi yao wanasema, "Peana mikono, nyunyizwa, ingia ndani ya kanisa, *hili* Ndilo, hilo ni lile." Mungu hana budi kuhukumu kanisa, ulimwengu, kwa kitu fulani. Kama Yeye anaenda kuuhukumu kwa kanisa, litakuwa kanisa gani? Kama Yeye akiuhukumu kwa kanisa Katoliki, kanisa Katoliki lipi? Akiuhukumu kwa Warumi, la Kiothodoksi limepotea. Na kama wakiuhukumu kwa la Kiothodoksi, Othodoksi ya Kiyunani, basi wengine wamepotea. Kama wakiuhukumu kwa la Kibaptisti, Methodisti imepotea. Kwa ninii . . . Maana, huwezi kuongeza neno moja, au kuondoa moja kutoka kwa Hilo. Unaona? Kwa hiyo, kumbuka, neno moja halikuaminiwa!

92 Neno moja lilisababisha kila huzuni, kila ugonjwa, kila kifo, na hata kuja kwa Bwana Yesu kufa ili kutukomboa.

Hawa, alikosa kuamini, alihojiana tu na Shetani, ama Shetani alihojiana naye. "Vema, *hilo,* kwa kweli, Mungu hatafanya hivyo."

93 Unaona, hiyo ndiyo shughuli ya Lusifa leo hii, sema, "Mungu hawezi kutukataa. Sisi ni watu wakubwa sana. Tunasimama makumi ya maelfu, mamilioni wenye nguvu. Unafikiri Mungu angeweza kutukataa?" Yeye, hakika, Yeye amefanya hivyo tayari. Wakati unapolikataa Neno Lake, uko upande ule mwingine. Siye Mungu anayekukataa; wewe umemkataa Mungu. Hapo ndipo lilipo. Unaona? Unaona?

94 Inakubidi kuchukua Mkate wa Uzima. "Mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa . . . " Maneno machache, neno moja mara kwa mara? "Kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu, mtu ataishi kwa Hilo." Na Andiko hili limeandikwa na Roho Mtakatifu, hiyo ni kweli, na Roho Mtakatifu ni Mungu. Na, kila, mtu huyu "alichochewa, mtaka-, na Roho Mtakatifu," aliandika Biblia hii. Nami ninaamini kila Neno Lake kikamilifu ni Kweli ya Mungu, na haliwezi kuvurugwa. Na sisi tutahukumiwa kwa Kitabu hiki, kwenye mwisho wa . . . wa safari ya maisha. Naam, bwana.

95 Siamini katika hotuba za kiakili. Ninaamini Neno Lenyewe, na halafu udumu na ahadi hiyo mpaka iwekwe dhahiri na kutimizwa, basi umeipata. Kitu gani? "Mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu."

96 Nilikuwa tu nikiwazia hivi majuzi. Biblia ilisema, kwamba, "Dhambi za Sodoma ziliitesa nafsi ya Lutu, kila siku." Niliwaza tu, ni Lutu wangapi walioko katika Marekani hii! Watu wanaketi katika chumba chao cha kusomea, watu wazuri, wakiketi katika chumba chao cha kusomea, wakiangalia nje kupitia dirishani, na kuona hawa wavua nguo mamboleo mtaani, na kufanya yasiyofaa, vile pale. Hawawezi kusema chochote kulihusu. Wanajua ni kosa. Hawawezi kusema chochote, nusu ya kusa- lao . . . naam, asilimia tisini ya kusanyiko lao huvaa hilo. Wanawake waliokatwa nywele, wakivaa kaptura, wanaume wanavuta sigara, wakinywa vileo, wakitoa mizaha michafu! Wanajua vyema zaidi ya kusema hayo. Wakifanya hivyo, makao makuu ya dhehebu lao, wanachochea kitu kama hicho, wanatengwa kutoka kwa hilo. Unaona, Lutu mamboleo bila ya ujasiri wa kawaida, bila Kweli halisi ya kiroho ndani yao, neema ya kutosha kusimama, ambaye ataitazama dhambi, na hawezi kuitaja.

97 Mungu, tupe Ibrahimu fulani watakaojitenga kutokana na mambo haya. Kweli. Loo, kwenye siku tunayoishi! Naam, bwana.

98 Neno Lake daima ni Kweli, daima ni Kweli. Watoto Wake waaminio wanaamini kwa ajili yake, na kulililia, mpaka Neno Lake liwe limethibitishwa. Na Neno Lake daima ni mapenzi

Yake. Kama ukitaka kujua kile mapenzi ya Mungu yalicho, yapate katika Biblia. Ni Neno la Mungu. Chochote kinyume na Hilo, kimepotoshwa. Na usiingie katika hali hiyo ya uchotara. Kile alichosema Mungu, hicho ndicho Kweli.

99 Mtu fulani akikuchukua, na kusema, “Sasa, ninakuja kanisani, na ninakwambia, hatuamini katika kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hatuamini hilo. Tunaamini kwamba wewe kwa kweli, unaamini, wakati ukiamini, unapokea Roho Mtakatifu.”

100 Paulo alisema, katika Matendo mlango wa 19, “Je! mmepokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?” Unaona? “Je! mmepokea Roho Mtakatifu?”

“Vema, ulipokeaje Roho Mtakatifu?” ulisema.

101 Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, kasema, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.” Hilo ndilo alilosema. “Ahadi ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu.”

102 Ni kama watu wanaosoma maagizo juu ya chupa ya dawa na hawatakunywa dawa. Inafaidi nini kusoma maagizo? Vema, wanaenda kwenye seminari, na kusoma historia ya kanisa, na tunasoma maadili ya kanisa, na kusoma kile Biblia isemacho, na maneno yote ya Kiyunani, na tunaweza kukuambia yanayomaanisha; lakini huko ni kukuambia tu kile chupa isemacho, kile maagizo yasemacho. Ninaweza kukuambia kile Petro alichosema kwenye Siku ya Pentekoste, ninaweza kukuambia kwamba ahadi ni kwa ajili yenu, bali wewe unasema, “Ninaamini Hilo.” Ninaweza kuamini dawa hii iliyowekwa hapa kwa ajili ya ugonjwa ni sahihi, bali, mpaka nitakapoimeza, inanibidi kuimeza! Unaona, u—uaminifu wake haujalishi. Unasema, “Kwa kweli ninaamini hilo. Hilo ni kweli.” Lakini inakubidi kulimeza. Na ukilimeza, linaonyesha matokeo juu ya mgonjwa. Na wakati ukilichukua Neno la Mungu, Hilo huonyesha matokeo halisi ya Roho Mtakatifu, kwa imani, Uzao wa Ibrahimu. Hukufanyia jambo fulani. Hukushika. Hutikisa kutokuamini kutoka kwako, na kuweka shauku zako kwenye mambo ya Juu.

103 Ambapo, Yesu alisema, “Nikiinuliwa, nitavuta watu wote Kwangu.” Na Yeye ni Neno. “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Neno lilikuwa pamoja na Mungu, nalo Neno lilikuwa Mungu. Nalo Neno likafanyika mwili likakaa katikati yetu.” Nalo Neno lingali ni Mungu. Basi Neno likiinuliwa juu, na upokee Hilo moyoni mwako, Hilo litakuvuta kwa Mungu. Hiyo ni kweli, kwa sababu Hilo ni Mungu. Amina. Loo, jinsi ninavyompenda Yeye. Neno daima ni Kweli. Naam, bwana. Kamwe hakuna njia iliyo bora kuliko njia ya Mungu iliyotolewa!

104 Kulikuwa na nabii, wakati mmoja, jina lake Ayubu. Alihitaji, a—alihitaji faraja fulani. Basi yeye . . . washiriki wa kanisa lake walikuja, na wakimlaumu, na wakisema, "Ayubu, unajua, wewe—wewe—wewe—wewe huko sawa tu na Mungu." Na—na wao wakamhukumu. Lakini bado alihitaji mfariji. Mke wake hata asingeweza kumfariji. Mke alisema, "Ayubu, unapaswa kumlaani Mungu, na ufe mauti."

105 Lakini alisema, "Wewe unaongea kama mwanamke mpumbavu." Na Ayubu akadumu nalo mpaka Mungu akampa ono la Yesu Kristo. Sasa, je! mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

106 Ilisema, wakati ono lilipokuja, alisema, "Ninajua Mkombozi wangu yu hai, na katika siku za mwisho Yeye atasimama juu ya nchi. Na ingawa mabuu ya ngozi yanauharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu; ambaye nitamwona mwenyewe, macho yangu yatamwona, mwingine."

107 Sasa kumbukeni, ono ni, alimwona Yesu. Na Yesu ni Neno. Basi wakati Ayubu alipohitaji mfariji, Mungu alimtumia ono la Neno. Amina. Whiu!

108 Hiyo ndiyo faraja ninayopata, ni kusoma Neno, kuamini Neno, kile Neno lisemacho. Yesu alisema, "Acha neno la kila mtu liwe uongo, na Langu liwe Kweli." Sijali kile mtu yeyote mwingine asemacho. Ni—ninaheshimu kile wasemacho. Lakini ikifikia kuamini, kama ni kinyume na Neno la Mungu, sikiamini. Siamini chochote ila kile Neno la Mungu lilichosema, kwa kuwa, "Mtu ataishi kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu," si tu kiasi fulani cha Neno. Alisema, "Neno lote," Biblia nzima kote. "Mtu ataishi kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Sasa, hivyo ndivyo mwanadamu aishivyo. Hiyo ndiyo njia ya Mungu iliyotolewa kwa ajili yake kuishi.

109 Na Ayubu alikuwa nabii aliyeishi hata kabla ya Biblia kuandikwa. Pia tazama, alikuwa nabii, nalo Neno la Mungu humjia nabii. Na basi wakati alipohitaji faraja, asingeweza kupata yoyote. Alienda kwenye kanisa lake, na kanisa lake haliku—halikuwa na faraja yoyote kwa ajili yake, ila lawama dhidi yake. Lakini yeye alikaa mpaka Mungu akamwonyesha Neno, kwa ono, ndipo akafarijika. Na yeye alikaa miguuni mwake, na umeme ukamulika na radi kunguruma. Ndipo yeye akasema, "Ingawa mabuu ya ngozi yanauharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu. Yeye alizungumza na mimi. Acha mauti au chochote kingine kinipige, haileti tofauti yoyote, maana nitamwona Mungu. Niliona ono la Neno Lake."

110 Israeli, siku moja, walikuwa Misri, huko chini katika utumwa. Na wao walihitaji njia, walihitaji njia ya kutoka Misri. Basi, angalia, tunapata kwamba mtu alifunzwa, jina lake Musa. Alifunzwa katika uwezo wote wa kijeshi, halifa wa Farao, huko

chini Misri. Alifunzwa katika uwezo wote wa kijeshi. Alidhania siku moja angeweza kuwakomboa watu Wake. Ndipo akatokea, mtu huyu mwenye nguvu, mwenye uwezo katika kunena na kutenda, Musa. Na yeye alijaribu kwa uwezo wake wa kijeshi, bali haikuwa njia ya Mungu iliyotolewa. Alikosa kitu fulani.

111 Lakini siku moja wakati alipokuwa upande wa nyuma ya jangwa, kile alichokosa, kichaka kilichowaka moto kilikuwa nacho. Na Musa aliona ono la Neno, hilo lilikuwa ni Mungu. Basi wakati alipoona, ono lilinena Neno. "Ninaikumbuka ahadi Yangu," amina, "kwa Ibrahimu, Isaka, na kwa Yakobo. Na ninakumbuka niliwaahidi, na nimeshuka chini ili kuwakomboa." Amina. Loo, jamani! Ndipo, kama nilivyozungumza hivi majuzi usiku kwenye Maskani, Musa alifanyika mfungwa kwa Mungu.

112 Isipokuwa Mungu aweze kukupata, mfungwa! Paulo alifanyika mfungwa. Unaona, huwezi kuangalia kile unachofikiria, huwezi kuangalia kile mtu mwingine anachofikiria. Inakubidi kuenda tu kile Yeye anachosema ufanye. Wewe ni mfungwa.

113 Paulo alijua kwamba alisukumwa katika roho kwenda mahali fulani, wakati yeye hakutaka kwenda. Alijua kwamba Roho alimzuia kuenda sehemu zingine. Alijua ilimbidi kutulia mara nyingi.

114 Maskini yule mzee mpiga ramli alikimbia nyuma yake siku moja, akipaza sauti kote nyuma yake. Naye Paulo, akiwa na huyo Roho wa Mungu, alitaka kuikemea, na siku baada ya siku. Na hatimaye alipata ujumbe, "Mkemee," ndipo akageuka. Asingeweza kufanya hivyo mpaka Mungu aliposema hivyo. Amina.

115 Loo, iwapo kanisa lingaliweza tu kuwa hivyo katika Uwepo mtukufu wa Mungu, siku moja Mungu atafungulia Nguvu Zake ndani Yake, mambo yatatendeka. Bali huwezi kuchanganya chakula chako; utakuwa chotara. Dumu hasa kile Mungu alichosema. Dumu moja kwa moja ndani ya Neno, na Mungu atathibitisha Hilo kuwa Kweli. Naam, bwana.

116 Mungu aliwapa Israeli njia. Alimtia upako nabii, akatuma Nguzo ya Moto, na kuthibitisha Neno ambalo nabii alinena, kwa ishara, kwa ishara za uumbaji. "Musa, nenda ukainyoshe fimbo yako juu ya bahari, nje kuelekea Mashariki, na useme, 'Hebu kuje nzi.'" Naye Musa, mtu aliye na Neno la Mungu, akijua kwamba mwanadamu hawezi kuumba, alichomeka ufito wake kuelekea Mashariki, namna *hiyo*, na kusema, "Kuwe na nzi kote katika Misri." Ndipo nzi, wakaumbwa, na wakaja katika uwepo kwa neno la mwanadamu.

117 Mungu humtumia mwanadamu kama chombo Chake. Yeye anaweza tu kunena kupitia mwanadamu. "Mimi ndimi Mzabibu, nyinyi ni matawi." Hiyo ni kweli. Alisema . . .

118 Hakukuwa na vyura. Alisema, "Musa, enda huko nje na uinue fimbo yako juu, na uite vyura." Hilo lilikuwa ni agizo la Mungu kwake.

119 Na Musa akasema, "Sasa ngoja kidogo, ngoja kidogo, sasa labda siku za hiyo . . . Sikuwahi kusikia kuhusu kitu kama hicho. Afadhali nitulie kidogo"? Hakuwa na madhehebu yoyote ya kiakili kumwambia cha kufanya.

120 Aliishi kwa ahadi ya Mungu. Alikuwa ni mfungwa katika nyumba ya Mungu. Angeweza tu kwenda na kufanya kama Roho alivyomjalia kufanya. Amina. Ndipo akainua fimbo, na kunena, na vyura wakaja katika uwepo. Hakika.

121 Walitoa mwana-kondoo wakati walipohitaji kitu kwa ajili ya dhambi yao. Njia iliyotolewa na Mungu ilimfanya mwana-kondoo. Njia ya Mungu iliyotolewa ilifanya njia kupitia Bahari ya Shamu walipokuwa ndani ya mtego. Njia ya Mungu iliyotolewa iliwapa nabii, iliwapa Nguzo ya Moto kuwafuata, thibitisho la Neno, mtu aliyethibitishwa na Mungu, kwamba kile alichosema kilikuja kutimia, kikamwonyesha kile hasa kilichokuwa. Na hata hivyo, walipovuka bahari, walitaka torati. Unaona, hao tu ni wanadamu. Hiyo tu ni vile mwanadamu hufanya, anataka kuingiza njia zake mwenyewe.

122 Loo, njia ya Mungu iliyotolewa daima ni njia ya kutuma Neno Lake.

123 Kifo kiliipiga Misri. Alikuwa anaenda kuua kila kitu katika Misri. Sasa kumbukeni, wakati majipu yalipokuwa yanatokea, wakati moto ulipokuwa ukishuka, na wakati mvua ilipokuja na mvua ya mawe kuja, Mungu alitoa mahali kwa ajili ya wateule Wake wasiingie katika hiyo. Alikuwa na mahali palipoitwa Gosheni. Sasa kulikuwa kunakuja roho wa mauti juu ya nchi. Basi kila mtu, kumbukeni, mauti ndiyo sababu tunakufa. Na Israeli ilibidi wawe na kitu cha kuwazuia kufa, ama kifo kingewapiga, pia. Maana, adha-, adha- . . . mshahara wa dhambi ni mauti, na Israeli ilikuwa imetenda dhambi. Basi Mungu, kusudi wasiweze kufa, watu Wake waliokuwa wanajaribu kumfuata Yeye, Yeye aliwatolea mwana-kondoo, na damu juu ya mlango, hiyo ilimlinda mzaliwa wao wa kwanza. Njia ya Mungu iliyotolewa. Wakati, Misri ilidhania wangeweza kujifungia ndani, kuzunguka wanatheolojia wao wote mashuhuri na waganga, na chochote walichokuwa nacho, ninii . . . na malaika wa mauti akafagilia moja kwa moja juu ya hayo, maana yalikuwa bila damu.

124 Na dini yoyote leo hii ambayo haina Damu Uhai wa Yesu Kristo nyuma yake, malaika wa mauti yuko juu yake; kweli, malaika wa mauti, wametengwa na Mungu. Naam, kweli, Ikabodi imeandikwa juu ya kila sehemu yake isiyo na Damu.

Unasema, "Vema, nina furaha, Damu!"

125 Kama Damu haijafanya kazi, kama haijafanya kazi na uione maishani mwako, kama mwana wa Mungu aliyewekwa wakfu, pamoja na kile ambacho Yesu alisema kingefanyika, basi kuwa mwangalifu, huenda ukawa na kitu kingine mbali na Damu. Huenda ukawa na kuingiza kidogo kwa theolojia hapo, ama kitu fulani, kuingizwa kidogo kwa msisimko. Unasema, "Nilitetemeka. Nilitikisika. Nilicheza densi. Nimefanya *hili*." Kuwa mwangalifu.

126 Dawa ikipata kukupiga, inafaa kwa kila mwanadamu. Itaokoa kutokana na dhambi. Itasafisha, kutokana na maisha ya dhambi. Itafanya mtu tofauti kutoka kwako. Itaondolea mbali shaka, na itakufanya kiumbe kipya ndani ya Kristo Yesu. Amina.

127 Kifo kiliipiga Misri. Mungu alitenganisha imani kutoka kwa kutokuamini, siku hiyo, kwa—kwa damu juu ya mlango.

128 Musa, mtumishi mwaminifu aliyefuata kila fundisho la Mungu, alipofikia mahali ambapo ilimpasa kufa. Alikuwa anazeeka sana, umri wa miaka mia moja na ishirini, ilimbidi kufa. Hakuwa na mahali pa kufia. Hakutaka kufia huko chini pamoja na hayo manung'uniko na kila kitu namna hiyo. Mungu alimtolea mwamba. Amina. Alianza kupanda, mpaka akafika juu ya kutokuamini kote, na Mungu alikuwa na mwamba uliokuwa umewekwa pale. Ndipo akafa juu ya huo mwamba, akitazama nchi ya ahadi.

129 Hapo ndipo mahali. Mwamba huo ni Kristo Yesu, anayekuelekeza kwenye nchi ya ahadi. Wewe panda juu Yake wakati mmoja, na utaona kila ahadi ya Mungu ni kweli. Kabisa. Hiyo ni kweli. "Mki—mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, basi ombeni mtakalo nanyi mtatendewa." Maana, Yeye ni Neno. Hujidhihirisha tu Lenyewe kupitia wewe, ukikaa ndani Yake.

130 Tazama, baada ya yeye kufa, alikuwa mbali huko juu nyikani, alihitaji wabeba jeneza. Mungu akatoa Malaika. Kwa nini? Kwa sababu hakuna mtu juu ya dunia hii angaliweza kumpeleka mahali alipokuwa anaenda. Ilihitaji mtu kumpeleka Huko, na ilichukua Malaika huko Nyumbani.

131 Henoko alihitaji ngazi, siku moja. Alikuwa ametembea miaka mia tano pamoja na Mungu, na alikuwa amempendeza Yeye. Alihitaji ngazi. Mungu alimpa barabara kuu, akatembea moja kwa moja akaenda Nyumbani.

132 Eliya alihitaji kamba, wakati mmoja, na Mungu akampa gari pamoja na farasi kwa ajili yake. Loo, jamani!

133 Samsoni alihitaji mkuki, na Mungu akampa mfupa wa taya la nyumbu wa mwituni, na akapiga na kuwaangusha Wafilisti elfu moja kwa huo.

Mungu hukupa mahitaji yako. Mungu anayo njia.

134 Vipi kama Sam—vipi kama Samsoni angalisema, "Sasa ngoja kidogo. Mfupa huu wa taya hauna makali. Si mkuki. Ziangalie zile chapeo kubwa nene walizovaa Wafilisti"? Aliichukua tu njia ya Mungu iliyotolewa, na kupiga moja kwa moja katika hiyo.

135 Hayo ndiyo yote unayohitaji, ni kuchukua kile Mungu asemacho. Na uanze kupiga na hicho, kwa nguvu tu uwezavyo, utajiweka huru baada ya kitambo. Naam, bwana. Naam.

136 Yoshua alihitaji daraja. Mungu alitoa ngu—nguvu, mlango wa kuzuia maji, mlango wa kiroho wa kuzuia maji uliozuia Yordani, kwa hiyo aliweza kuendelea na kutimiza Neno la Mungu, ahadi. Alihitaji daraja.

137 Danieli alihitaji uzio, kumkinga na simba. Mungu alimpa Malaika. Unaona, hiyo ndiyo njia ya Mungu iliyotolewa. Kilichohitajika, Mungu alitoa, na Mungu alikitoa kwa njia Yake Mwenyewe.

138 Sasa vipi kama Danieli angalisema, "Sasa ngoja kidogo. Ninaweza kuwazia njia bora kuliko hiyo Nguzo ya Moto inayosimama hapa mbele zangu sasa. Huyo, huyo simba, huenda asiwe na madhara yoyote kwake. Huenda akapita moja kwa moja kwenye hiyo Nguzo ya Moto. Iwapo Wewe utanipatia tu uzio mkubwa mnene na kunizingira ndani"? Unaona, hiyo ingekuwa ni Danieli akijaribu kufanya jambo.

139 Lakini yeye alikubali tu njia ya Mungu iliyotolewa, akalala chini na kupatwa na usingizi, akalala usiku wote, kwa utulivu kabisa. Mungu alitoa njia. Naam, bwana. Loo, jamani!

140 Watoto wa Kiebrania walihitaji maji, mpira wa zimamoto huko chini, kuzima moto huo wote waliporuka huko ndani. Bali Mungu aliwapatia Mtu wa nne. Naam, bwana. Huyo tu ndiye waliyemhitaji.

141 Vipi kama wakisema, "Sasa ngoja kidogo, mtu mwingine tu aingie humo ndani, hiyo haitasaidia. Inabidi tuwe na mpira wa zimamoto kuzima huu wote"?

142 Walikubali njia ya Mungu iliyotolewa, na Yeye akawakinga na moto. Hakukuwa hata na harufu ya moto juu yao. Walipitia njia ya Mungu iliyotolewa.

143 Mamajusi walihitaji dira kuwaelekeza kwenye Mtoto mgeni aliyezaliwa, bali Mungu aliwapatia Nyota. Unaona? Walichukua Nyota. Hiyo ndiyo yote waliyohitaji.

Ulimwengu ulihitaji Mwokozi. Mungu akatoa Mwana. Amina.

144 Kanisa lilihitaji nguvu. Mungu akatoa Roho Mtakatifu. Hakutoa kitabu cha maadili. Hakutoa utawala wa Kikristo. Alitoa Roho Mtakatifu. Huyo ndiye Mungu alimtoa. Kamwe hakusema, "Nendeni huko juu na msome katika Yerusalemu huko juu, mpaka nipate kiasi fulani cha elimu ndani yenu, mpaka niwajaze kasumba, na *fulani na fulani*." Yeye alisema,

"Ngojeni mpaka mjazwe na Nguvu kutoka Juu. Baada ya Roho Mtakatifu kuja juu yenu, ndipo mtakapokuwa mashahidi Wangu katika Yerusalemu, Samaria, katika Chicago, Illinois, na kadhalika, mnaona, ulimwenguni kote." Huyo ni shahidi wa Mungu aliyetolewa, ni Roho Mtakatifu. Mungu hakuwapa kitabu cha maadili. Hakuwapa dhehebu.

Walisema, "Tunataka kuwa Wakristo kamili."

145 "Vema, sasa nyinyi ngojeni mpaka msome kwa muda mrefu, ngojeni mpaka mjifunze kanuni za imani"? Hakusema ujifunze chochote. Alisema, "Ngojeni mpaka mjazwe." Amina.

146 Mtu fulani alisema hivi majuzi, kasema, "Kwa nini, Bw. Branham, huamini katika madhehebu?"

147 Nikasema, "Sina chochote dhidi ya watu ndani yake, bali kwa kweli siamini katika mifumo yao."

Akasema, "Vema, kwa nini? Tungelipaje? Tutafanya nini?"

Nikasema, "Hiyo haikuwa njia ya Mungu iliyotolewa kwa kuanzia."

Akasema, "Wewe ni wa dhehebu gani?"

Nikasema, "Hakuna."

Kasema, "Wewe ni wa kitu gani?"

Nikasema, "Ufalme."

Kasema, "Unaingiaje ndani Humo?"

Nikasema, "Unazaliwa ndani Yake." Amina.

148 Unazaliwa ndani ya Ufalme wa Mungu. Kwa njia gani? Kwa Roho Mtakatifu. Huyo ni shahidi wa Mungu. Yeye hutoa ushahidi kwa Neno la Mungu, kwamba tumepita kutoka mauitini kuingia Uzimani, kwa sababu tuko ndani ya Ufalme wa Mungu. Kwamba Mungu . . .

149 Mungu alihitaji kiongozi kwa ajili ya Kanisa. Hakumwelimisha askofu, wala Yeye hakutuma kuhani mkuu au papa, au mtu yeyote mwingine. Bali Yeye alimtuma Roho Mtakatifu. Mtu anakufa, na mifumo yao inakufa, na kila kitu kingine. Lakini Roho Mtakatifu ni Mungu wa Milele, na Yeye hawezi kufa. Aliwapa Kiongozi wa Milele, na huyo ni Roho Mtakatifu. Walihitaji kitu fulani kuwaongoza, kuwaambia cha kufanya, jinsi ya kuishi, jinsi ya kukabiliana na umma, jinsi ya kukabiliana na ukali wa siku hiyo, jinsi ya kushinda ugonjwa, jinsi ya kushinda *hili,* jinsi ya kushinda dhambi. Mwanadamu amebuni kila namna ya njia za kujiunga na *hili,* na kanuni za imani ya *hili,* na stakabadhi za *hili,* na mabatizo ya *hili,* na kila namna ya misisimko, na mitetemeko midogo na hisia za kiajabu, na kila kitu kingine. Lakini bado inabaki, Roho Mtakatifu ndiye njia ya Mungu iliyotolewa kwa ajili ya Kanisa Lake. Amina.

150 Na Roho Mtakatifu ni Mungu, na Mungu ni Neno. Roho Mtakatifu ni Neno hili likithibitishwa kikamilifu.

Roho Mtakatifu ndiye kitu ambacho hulipa uhai Neno hili lililoahidiwa.

151 Unasema, "Nimekuwa na hisia." Kama haithibitishi Neno hili, sahau hisia hiyo. Naam, bwana.

152 Unasema, "Vema, nimefanya *hili*. Nimefanya *lile*. Na nimebatizwa *hivi*, *vile*."

153 Sijali kile umefanyiwa. Ikiwa Roho Mtakatifu yuko juu yako, Neno hili linathibitishwa kupitia wewe. Kwa sababu, Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa ulimwengu wote, na kila kiumbe." Amina. Njia ya Mungu iliyotolewa!

154 Miaka elfu mbili! Hilo lilienda sawasawa kwa yapata miaka mia tatu, ndipo wakawa na mkutano wa baraza wakati mmoja, huko Nikea, Rumi, na walitaka kuingiza kitu fulani. Ndipo baada ya Martin Luther, malaika mwingine wa Mungu alileta ujumbe, ndipo wakawa na kuingiza kwingine. Ndipo basi baada ya John Wesley, walikuwa na kuingiza kwingine. Na waliendelea tu kadhalika, mkutano wa baraza, mpaka wakapata mahali hapa, mpaka makanisa yamekuwa chotara kwa maadili ya mafundisho ya mwanadamu, na kuna uasi mkubwa sasa.

155 Kanisa linahitaji ishara ya Kimaandiko, Kweli, katika siku hizi za mwisho. Linahitaji kitu fulani.

156 Yaangalie madhehebu mbalimbali, upotovu; tunapofunga sasa, kabla hatujakuwa na mstari wa maombi. Angalia upotovu wa Maandiko. Wazia madhehebu yetu mbalimbali. Wazia njia zetu za Kipentekoste. Wazia Baptisti yetu, Presbiteri yetu, Lutheri yetu, hata kwa Huru zetu, chochote zaidi. Mtu hajui mahali pa kusimama.

157 Kanisa linahitaji, leo hii, thibitisho la Kimaandiko. Yesu alisema nini katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 14 na kifungu cha 12? "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo yeye atazifanya pia. Mambo yale yale niyafanyayo yeye atayafanya pia." Tazama, Yeye aliahidi, "Kama ilivyokuwa katika siku za Yona, nabii, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Unaona? Alisema, "Kwa kuwa kama Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi, siku tatu mchana na usiku, na alifufuliwa kama aliyetoka kwa wafu, hiyo itakuwa ishara kwa kizazi kiovu na cha zinaa."

158 Sasa, tunaishi katika siku za mwisho, pamoja na ishara iliyoahidiwa ya ufufuo. Baada ya miaka elfu mbili ya kutiwa kasumba na kuvutwa kutoka barabarani, na *huku*, na *kule*, mpaka watu hawajui cha kufanya. Bali Yesu aliwaambia, na kuwaahidi, "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu na Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu."

159 Ilinganishe leo hii. Chukua Mwanzo 6, na uangalie kile Yeye alichosema; jinsi ambavyo "watu mashuhuri," jinsi ambavyo

"wanawake wangekuwa warembo." Tuna kundi la wanawake warembo kuliko wote waliowahi kuweko duniani, tangu wakati huo. Wanawake wamekuwa warembo kuliko walivyokuwa miaka iliyopita. Wanavyo vitu vingi mbalimbali kuwafanya warembo. Rangi nyingi mbalimbali na poda na mapambo na mitindo ya nywele na kila kitu, na mavazi ya kizinifu na kadhalika, mpaka wanawafanya wa kuvutia.

160 Mwanaume alinijia jana, akasema, "Nina mvulana, miaka kumi na sita, Ndugu Branham. Nina mvulana, miaka kumi na miwili. Ninawapeleka nje mtaani, hawa maskini wavua nguo huku nje." Akasema, "Wavulana hao, ni wanaume wadogo," akasema, "niwaambie nini?"

161 Nikasema, "Bwana, sijui. Wapeleke kwa Kristo, na uwaache waokolewe na kujazwa na Roho Mtakatifu, na watageuza vichwa vyao kwa hao wavua nguo mamboleo."

162 Kumbuka, wakati wana wa Mungu walipowatazama binti za wanadamu na kuona kuwa walikuwa warembo, walijitwalia wanawake, wakajichukulia wanawake. Angalia hapa kwenye kashfa hii kubwa Uingereza, angalia kote katika Marekani, waangalie wasichana hawa makahaba katika U.N., kila kitu kingine, loo, ni mbaya sana. Na jambo ndilo hilo, wanaume "wenye sifa." Tumerudi moja kwa moja katika majira hayo, taa nyekundu zinamulika kila mahali, kuja kwa—kwa Bwana. Na Yesu akasema, "Kama ilivyokuwa kabla ya kuteketezwa kwa Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu." [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Hiyo ni kweli.

163 Wanawake wanakuwa hivyo, hawatambui kile wanachofanya; roho mwovu juu yao. Ni kwa nini mwanamke avue nguo zake namna hiyo, kujianika mwenyewe? Hamaanishi kuwa mbaya, wao—wao, wananaswa tu katika mtego huo, na wao hawajui hilo. Unaona, kama tu ilivyokuwa huko nyuma katika wakati huo. Mwili wa mwanamke unaanikwa kila mahali, unaona, wenye kuvutia sana, huwavuruga akili wana wa Mungu, karibu, na halafu sheria ya Sodoma na Gomora kumlinda na hiyo. Ni aibu jinsi gani, na serikali yetu inatetea upuuzi kama huo!

164 Laiti ningalikuwa gavana kwa muda mfupi, au kuwa na taifa hili. Kama ningemkuta mwanamke amevalia namna hiyo, angeenda kwenye jela ya wanawake kwa kifungo cha maisha. Kamwe asingeweza . . . Naam. [Kusanyiko linashangilia.—Mh.] Kama ningalimshika mwanamke na mwanaume namna hiyo, . . . ? . . . [Kusanyiko linashangilia.] Kama mwanamke na mwanaume walishikwa wakiishi namna hiyo, wote wawili wangekuwa tasa, ni hayo tu kwa hilo; na kufanywa moja kwa moja hadharani, na madaktari. Naam, bwana. Sisi tungeweka . . .

165 Adhabu ni maskini ninii tu ya kale. . . Sheria ni nini bila ya adhabu? Adhabu ya sheria ya Mungu ni mauti. Dhambi ni mauti. Hiyo ni kweli. Tunahitaji sheria ambayo ni kali. Sisi . . . Loo, jamani! Lakini kile tulicho nacho sasa, lundo la siasa, unaweza kuyumbishwa katika njia yoyote utakayo. Kitu chote kimepotoka.

166 Hima, kanisa, rudini kwenye Neno la Mungu aliye hai! Ishi kutokana na Hilo, na Hilo pekee, maana Hilo ndilo watu wa Mungu wanapaswa kuishi kwalo.

167 Mungu aliliahidi kanisa hili ishara ya Kimaandiko. Alisema ufufuo ungezalishwa tena, Yesu Kristo na Kanisa Lake watakuwa hata watakuwa kitu kimoja, katika siku za mwisho. Aliahidi hilo. Sasa tunajua kwamba ni kweli.

168 Sasa, Yeye pia aliahidi kwamba kutakuwa na kurejeshwa kwa Imani. Tunasoma katika Yuda, alivyosema katika Yuda, "Mwishindanie Imani iliyokabidhiwa watakatifu mara moja." Sasa tumeahidiwa, katika Malaki 4, kwa mfumo ule ule ambao Yeye alifanya daima, kwamba sisi tungerejeshwa kwa ile Imani ya asili. Loo, loo, jamani! Kurudi kwenye Mbegu ya asili, kurudi kwenye Mbegu kama ilivyoanza kwenye Siku ya Pentekoste, kurudi kwenye Mafundisho yale yale, Neno kwa Neno, nguvu kwa nguvu, Roho kwa R-. . . kitu kile kile, hasa kabisa kama ilivyokuwa huko mwanzo, kupitia ishara na maajabu ya Uwepo ulio hai wa Yesu Kristo. Baada ya miaka elfu mbili, Yeye angali hai. Na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.

169 Nilimwambia Billy, "Kwenye dakika thelathini, nitupie kitu fulani, nitaacha kuhubiri." Sasa nimepitisha wakati huo. Tazama, ninapata tu . . .

170 Ninajua mimi si-. . . hatuna muda mwingi zaidi, wakati umewadia.

171 Marafiki, msije tu kwenye mkutano, useme, "Vema, niliifurahia sana. Kulikuwa na joto kidogo, bali niliifurahia." Usifanye hivyo.

172 Kuwa mwaminifu. Ingia ndani yake. Fanya maungamo. Jisafishe. Iwapo kuna mashaka madogomadogo na kuvunjika moyo moyoni mwako, hata usije kwenye mstari wa maombi. La, bwana. Ninataka safi. Maungamo yetu ni njia ya mzunguko.

173 Nilikuwa na mwanamke katika usaili hapa, majuma machache yaliyopita. Na yeye akasema . . . nilipata hapo ambapo alikuwa na mtoto, alikuwa wa mwanamume mwingine. Na yeye alikuwa ameishi na wavulana wawili, na alikuwa amechukua mvulana huyu mmoja na kuolewa naye kwa sababu alimpenda zaidi, na akasema mtoto alikuwa ni wa huyo mvulana. Huku akijua muda wote kwamba alikuwa wa mtu mwingine.

Ndipo akasema, "Niliungama hiyo."

174 Nikasema, "Naam, hivi ndivyo ulivyolisema. 'O Mpenzi, O Mpenzi, vipi kama uliwazia jambo fulani, O Mpenzi? Unajua, maskini John, shahibu, shahibu, vipi—vipi kama ningekuambia mtoto huyu alikuwa ni wa mtu mwingine? Hee-hee, usingeamini hilo, sivyo?' 'La.' 'Vema, vipi kama ilikuwa? Loo, sema, John, hivi tunaenda nje usiku wa leo kula hambaga?'" Hayo si maungamo. Enda magotini mwako!

175 Hivyo ndivyo watu humjia Mungu. "Ee Bwana, Wewe ni mwema sana, Wewe huniacha tu nifanye chochote nitakacho." Usiamini hilo. Mungu ana sheria unayoishi kwayo. Mpaka ujisafishe, na kuosha, na kukiri, na kuamini kwa moyo wako wote, na kurudi kwenye Neno la Mungu, wewe ungali mwenye hatia. Huwezi kufanya hivyo.

176 Inakubidi kukirarulia mbali kitu hicho. Watu inabidi waje, watauwa, waaminifu, waende chini magotini mwao na wabaki hapo mpaka matokeo yatokee, acha hiyo nguvu ya Roho wa Mungu ya upendo wa Mungu iingize moyoni mwako na kukufanya ukiri dhambi zako zote na kutokuamini kwako kote, na kumkubali Yesu Kristo.

Mungu ametuma kila kitu Yeye alichoweza.

177 Angalia jinsi ambavyo Yeye alithibitisha hilo mara ya kwanza, kama Ndugu Vayle alivyokuwa akisema muda mfupi uliopita. Unaona? Walijuaje Yeye alikuwa Masihi wakati Yeye alipomwona yule mwanamke kisimani? Alimwambia kilichokuwa shida yake. Upesi, mwanamke huyo katika hiyo hali mbaya, akiishi na waume sita. Kasema, "Umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako." Waume sita, waume sita katika mlolongo, alikuwa anatembea nao, katika hali hiyo.

178 Lakini wakati alipoambiwa, aliona kwamba Neno la Mungu, kali kuliko upanga ukatao kuwili, mtambuzi wa mawazo ya moyoni, akasema, "Bwana, hapana shaka Wewe ni nabii." Sasa, Neno la Bwana humjia nabii, unaona, kufunua mambo haya. Kasema, "Hapana shaka Wewe ni nabii. Hatujakuwa na manabii kwa mamia ya miaka. Bali," kasema, "Hapana shaka Wewe ni nabii. Sasa tunajua kwamba tunamtazamia Masihi, na, ajapo Masihi, hayo ndiyo Yeye atakayofanya."

Yesu akasema, "Mimi Ndiye."

179 Ndipo watu wa mjini, wa mji huo wote wa Sikari, kila mtu alimwamini Yesu Kristo. Haikumbidi kufanya hivyo tena. Aliifanya mara hiyo moja, na kila mtu alimwamini Yeye kwa sababu mwanamke huyo alisema hivyo. Ushuhuda wake, alikuwa amebadilishwa hivyo, wasingejizuia kuamini hilo. Loo, tupe wanaume na wanawake walio na shuhuda chanya, ambao watawaleta watu kwenye toba tena. Walimwamini Bwana Yesu Kristo.

Sasa, kwa ishara hiyo, Yeye alithibitisha kuwa Yeye alikuwa ni Masihi.

180 Mungu, nisaidie, kwa ishara ile ile, pamoja na Roho Wake, kuthibitisha kwamba Yeye angali Masihi. Amina. Ni kwa Neno la Mungu pekee ambalo tutaishi. Ahadi yake ni kwamba Yeye atafanya hivyo.

181 Sasa kubali njia ya Mungu iliyotolewa kwenye wakati wa mwisho. Kama wewe ni mgonjwa usiku wa leo, Mungu anayo njia iliyotolewa. Yesu Kristo ndiye njia iliyotolewa. Kama wewe ni mwenye dhambi, usiku wa leo, huamini, huwezi kuishi sahihi, huwezi kupata kutulia; Yesu Kristo ni njia ya Mungu iliyotolewa. Mwamini tu Yeye. Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Ndipo Yeye, katika Roho Mtakatifu... Ambaye Ndiye, Roho Mtakatifu ni Yesu katika (Kristo) katika umbo la Roho. "Kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena, hata hivyo nyinyi mtaniona Mimi, kwa kuwa *Mimi* nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu..." Roho Mtakatifu: Kristo akimwita Huyo *Mimi*. Unaona? Kristo, Mungu, Roho Mtakatifu ndani Yake, alikuwa awe ndani ya Kanisa Lake, "...hata mwisho wa ulimwengu." Neno la Mungu. "Nazo kazi nizifanyazo nanyi pia mtazifanya. Kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena, bali nyinyi mtaniona Mimi, kwa kuwa ninaenda kuwa ndani yenu. Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo mimi yeye pia atazifanya. Ndani yenu, hata mwisho wa ulimwengu." Mungu anayo njia iliyotolewa kwa ajili ya watoto Wake waaminio. Yesu Kristo ndiye hiyo njia, yeye yule jana, leo, na hata milele.

Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi.

182 Huku mmeinamisha vichwa vyenu, je! mnaamini kwamba Yeye ndiye njia? Je! kuna wengine hapa ambao wangependa kuamini hilo, na kamwe hawajalikubali bado? Rafiki, hivi utainua mkono wako, uwe mwaminifu hivyo hapa katika ulingo huu wa kale, usiku wa leo, na useme, "Ndugu Branham, niombee. Sitaki, si—si—sitaki kukutana na Mungu hivi"? Pia kumbuka...

183 Tulikatiza mazungumzo, kuchukua simu mahali fulani, hivi majuzi. Na mwanamke huyo alikuwa ndiyo kwanza aingie, na mwanaume alikuwa anampigia simu, aliyekuwa nje pamoja naye, na mwanamke huyu anadhaniwa kuwa ni Mkristo. Ndipo akasema, "Je! mume wako angali amelala?" "Naam." Kasema, "Kama akiwahi kugundua, sisi..." Kasema, "Haileti tofauti yoyote kwangu mimi," na mtoto mchanga akilia.

184 Je! mnatambua? Hivi mnaweza kuelewa? Ulimwengu huu wenye zinaa, mchafu, wenye kinyaa, yuko katika mwisho. Mungu anaenda ku...

185 Hakutakuwa na jengo moja litakalokuwa karibu na jingine, katika Chicago mojawapo ya siku hizi, au hakuna mahali popote pengine. Mungu anajiandaa kuumwaga ule muhuri wa sita juu

ya nchi, avunje muhuri huo na kuachilia ghadhabu ya Mungu juu ya nchi. Lakini kabla Yeye hajafanya hivyo, Kanisa litakuwa limeondoka. Bibi-arusi atakuwa ameenda; kanisa halitaninii, atapitia kwenye dhiki kuu, bali Bibi-arusi atakuwa ameenda. Maskini mke Wake hatapitia hiyo.

186 Hivi hutaki kuwa mmoja wa hao washiriki Wake, usiku wa leo? Kama unataka, na unataka kukumbukwa katika maombi, huku umeinamisha kichwa chako, inua mkono wako. Mungu akubariki. Mungu akubariki, na wewe, na wewe.

187 Baba yetu wa Mbinguni, maneno yote niliyoweza kusema, yasingemaanisha chochote yakilinganishwa na Neno moja ambalo Wewe ungesema. Mimi ni mwanadamu tu nikinukuu yale Wewe uliyosema. Ninaomba kwa ajili ya hawa walioinua mikono yao. Mungu, tujalie.

188 Ono hilo kubwa, asubuhi ya leo, lilinivuruga kabisa, Bwana. Ningali nimevurugika. Na mimi ninaomba kwamba—kwamba Wewe utanisaidia, nitulize, Bwana. Nina wasiwasi, na ninaomba kwamba—kwamba Wewe utasaidia.

189 Kama kuna hawa walioinua mikono yao usiku wa leo, walioingia kwa bahati katika jengo hapa, kwa njia fulani, jalia Roho Mtakatifu mkuu awanenee sasa, na jalia waje Kwako kwa utamu. Ninajua desturi ni kwamba, Bwana, kuita watu karibu na madhabahu. Tunaamini hilo ni sawa. Bali kulingana na Maandiko, walisema, "Wote walioamini, walibatizwa."

190 Na mimi ninaomba, Mungu, ya kwamba watu hawa wangeharakisha kwa ajili ya ubatizo wa Kikristo, wakikuamini Wewe, na kukiri dhambi zao, na kumkubali Yesu Kristo na Damu Yake kwa ajili ya msamaha wao, halafu wasimame na kubatizwa, wakiliitia Jina la Bwana, akiosha na kuondolea mbali dhambi zao. Na tena naomba wajazwe na Roho Mtakatifu wa ahadi Yake, watiwe muhuri, ule Uzima ambao hubadilisha asili yao yote, huwapa tumaini jipya, huwafanya watazamie; wanakuwa mfungwa, kutokana na shauku yoyote, nia zozote.

191 Kama vile Mtakatifu Paulo mashuhuri, alitaka kuwa rabi. Alitaka kuwa mtu mashuhuri. Alielimishwa. Baba yake na mama walimwelimisha kuwa hivyo. Na huko nyuma upande wa nyuma ya lile jangwa, baada ya kukutana na ile Nguzo ya Moto siku hiyo, iliyokuwa imemwambia, "Ni vigumu kwako kupiga mateke vichokoo." Kaita jina lake, "Sauli, Sauli!" Nguzo ya Moto ingewezaje kuita jina lake? Bali Yeye akasema, "Mimi ni Yesu." Na yeye akajua kwamba hilo ndilo Yesu alilotenda wakati Yeye alipokuwa hapa duniani. Alijua hiyo Nguzo ya Moto ilikuwa ndiyo Kristo aliyewaongoza watu wake kutoka Misri, kupitia nyikani, na alijua kuwa Hiyo ilikuwa ingali ni yule aliyepakwa mafuta.

192 Tena, Bwana, tunajua Wewe ungali yeye yule leo hii. Ninaombea kila mmoja. Wape amani mioyoni mwao, Bwana.

Litakase kanisa hili dogo, na uwajalie wote wanaohusiana nalo, na wageni wote malangoni petu, kwa ajili ya Yesu ninaomba hayo.

193 Na halafu, Baba, ninaomba pia kwamba Wewe utawaponya wagonjwa. Thibitisha yale ambayo nimesema, kuwa ni kweli. Muda wangu unakwisha, Bwana, ninazeeka, na ninaomba kwamba Wewe utanisaidia kushawishi kila nafsi niwezayo. Pia, Mungu, wajalie watu waone, usiku wa leo, kwamba Mwenyezi Mwenyewe akishuka chini miongoni mwetu na kuthibitisha kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, hebu watu waone kwamba, "Mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Tujalie, Bwana. Na wasijichanganye wenyewe na maambukizo fulani makubwa ya—ya kijidudu cha ugonjwa fulani ambacho huleta kutokuamini moyoni mwao, bali hebu maambukizo hayo yaondolewe na nguvu za Roho; na mbegu ya Uzima wa Milele iishi ndani yao, kusudi waweze kukua kufikia kimo kamili cha Yesu Kristo, kwamba, katika siku hii ya mwisho, kwamba Yeye na mke Wake waweze kuwa kitu kimoja. Tujalie, Bwana. Ninaomba katika Jina la Yesu. Amina.

194 Sasa aminini, enyi watu mlioinua mkono wenu. Ukimwamini Bwana Yesu Kristo, na kumkubali Yeye kama Mwokozi wako, na kumwamini Yeye, kwamba Damu Yake, na hiyo pekee, huondoa dhambi yako, basi ninataka uone baadhi ya hawa wahudumu hapa, kwa ajili ya ubatizo moja kwa moja. Watakuambia cha kufanya kuanzia hapo.

195 Sasa kwa wagonjwa na wanaoteseka, wale walio na kadi za maombi, hebu tuanzie namba moja, na tuanze na kuwaleta wachache wa hao hapa juu, nasema yapata moja hadi kumi na tano. Nimechelewa yapata dakika kumi na tano, ishirini. Ningepaswa niwe nimeondoka, dakika kumi na tano, ishirini zilizopita.

196 Namba moja, ni nani aliye nayo, kadi ya maombi namba moja? Inua mkono wako, yeyote yule aliye na kadi ya maombi namba moja. [Ndugu Lee Vayle anasema, "Je! ingekuwa bora kama wangesimama, ndugu, kusimama?"—Mh.] Simama, yeyote yule aliye na kadi ya maombi namba moja. Kama unaweza, simama. Hatuwezi kuona vizuri sana hapa, ni hali ya mwanga si nzuri. Kadi ya maombi namba moja, namba mbili, namba tatu, namba nne, tano, sita, saba, nane.

197 Ninii yetu . . . mama fulani hapa, huku mnapo- . . . Moja hadi kumi na tano, simameni sasa, huku wengine wetu tukiinamisha vichwa vyetu. Njoo moja kwa moja hapa, njoo papa hapa, namba moja hadi kumi na tano, huku tukiinamisha vichwa vyetu na kumwombea mama huyu, kwamba yeye ni mgonjwa hapa. Bibi Way anaye hapa, sasa, huku tukimwombea tena. Kuna joto sana humu ndani, usiku wa leo, jasho linajaa tu katika viatu vyangu.

Hebu tuombe sasa, sote tukiwa tumeinamisha vichwa vyetu.

198 Baba yetu wa Mbinguni, tujalie baraka hizi, katika Jina la Yesu Kristo Mwana Wako. Jalia neema na rehema, amani, msaidie dada yetu mpendwa, Mungu, kwa kuwa yeye ni mgonjwa na mhitaji. Jalia Roho Mtakatifu aje juu yake, Baba, na umpe, tena, afya njema tena. Yeye ni mgonjwa; amekuja kanisani, usiku wa leo, anataka kuifurahia, na hapa tunamwona ameketi hapa mgonjwa, anazimia, kwa sababu ya joto la hali ya joto kanisani. Mungu, mjalie uponyaji. Ninaomba baraka hizi katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

199 Vema, Bwana abariki sasa. Amini. Nilimwona akiitikia Dada Way kwa kichwa. Yuko peke yake sasa. Na sasa ikiwa baadhi yenu mnataka kumpeleka huko nje mahali anaweza kupata hewa kidogo. Kuna joto sana. Laiti ungesimama tu hapa na kujua kile—kile kinachomaanisha wakati huu sasa!

200 Sasa, hebu tuone, una wangapi? [Ndugu Vayle anasema, "Kumi."—Mh.] Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba. Vema.

201 Hebu tupate kuanzisha mstari wa maombi. Sasa kila mtu kuwa tu na kicho uwezavyo. Sasa kila mtu awe akiomba. Huku, mpiga piano akitupa sauti hapo, kama utaweza.

Amini tu, amini tu,
Mambo yote yawezekana, amini tu.

202 Hilo ni jema. Sasa kila mtu kwa kicho na katika maombi sasa. Vema. Sasa msisogee huku na huku tena. Msisogee. Msisogee. Enyi watu mnaoingia na kutoka, msifanye hivyo, unaona, maana hii ni hatari sana, unaona, hatari sana, sana. Vema. Sasa kila mtu tulia, na uombe, na uamini sasa kwa moyo wako wote.

203 [Ndugu Vayle anasema, "Tumekosa wanne."—Mh.] Unasemaje? ["Wanne wamekosekana."] Vema, hawaitikii mwito wao, hayo ndiyo yote nijuayo; walikosa kuitwa. Vema.

204 Ni wangapi waliokosekana? Mbili haipo, namba mbili? Ni nani aliye na kadi ya maombi namba mbili? Je! kuna watu hapa wanaoongea lugha nyingine kando na Kiingereza? Kadi ya maombi namba mbili?

205 Mvulana huyo huzichanganya tu hizo kadi na kuzigawa, hizo, mtu yeyote anazipata. Usiichukue kama huji. Unaona? Huna budi kuja huku, ikiwa unakuja. Usimpe mtu yeyote mwingine; inakubidi kuja mwenyewe.

206 Kadi ya maombi namba mbili? Vema, kama haipo hapa, hebu tuinamishe vichwa vyetu. Kuna joto sana, joto sana, sana. Na labda mama huyu hapa anayo. Je! unayo kadi ya maombi namba mbili, mama? Una kadi ya maombi namba mbili? Labda ni Mnorwe au kitu kingine, na hazungumzi. Billy, angalia kadi hiyo hapo chini, mtu fulani, na uone kama anayo kadi namba mbili.

Naam. Sasa . . . [Mtu fulani anasema, “Naam.”—Mh.] Namba mbili. Vema.

Namba moja, mbili, vema. Naam. Sawa, sasa, moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi. Kuna mbili au tatu zaidi ambazo zimekosekana. Moja hadi kumi na tano, mkiweza.

207 Vema, kila mtu awe na kicho sasa, unaona. Vema, sasa iweni na kicho kabisa, na mwombe sasa. Ni wangapi watakaokuwa wanaomba? Inueni mikono yenu, “Nitakuwa ninaomba. Nitakuwa ninaomba, nikimwamini Mungu.”

208 Sasa ni wangapi hapa nje ambao hawana kadi ya maombi, na unajua Mungu anaenda kutimiza, atakuponya, hebu tuone mkono wako. Wewe, wewe amini Mungu atakuponya. Kila mtu, vema, kila mahali sasa, kila mmoja aamini. Kuwa tu na imani. Usitie shaka. Mwamini Mungu, kwa moyo wako wote. Vema.

Njoo, mama.

209 Kwa namna fulani inafanya kila mtu kuharakisha na kusisimka, na Roho wa Bwana hapendi hayo hata kidogo. Unaona? Hebu tunyamaze, unaona. Nyamaza mwenyewe, useme tu, “Bwana, mimi hapa, nipo hapa kukutumikia Wewe. Ninakupenda, na ninajua Wewe utanipa haja yangu.” Jambo ndilo hilo.

Sasa je! mnaweza kunisikia? Nitajaribu kusimama papa hapa.

210 Mama fulani hapa. Hii hapa picha nzuri ya Biblia tena. Huyu hapa mama ambaye ni mama mweusi. Mimi ni mzungu. Kwa hakika inaleta picha nzuri ya Biblia, kwenu enyi wageni,

211 Yesu alikutana na yule mwanamke kisimani. Mwanamke huyo alikuwa Msamaria, Yeye alikuwa Myahudi, na wakaanza kuongea. Yeye akasema, “Nipe maji ninywe.” Akaanza kuzungumza naye, na Yeye akagundua kilichokuwa shida yake. Lakini kwanza Yeye alimwomba mwanamke huyo ampe maji anywe, na mwanamke huyo asingekubali, kwa sababu alikuwa ni wa jamii nyingine. Ndipo Yeye akamfanya mwanamke kujua, moja kwa moja, hakukuwa na tofauti katika jamii.

212 Na sisi hapa, usiku wa leo, baada ya miaka elfu mbili. Sasa, Yesu Kristo aliahidi kwamba mambo ambayo Yeye alifanya, mwaminio angeyafanya pia. Je! hiyo ni kweli? Sasa, kila mtu anaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Yohana Mtakatifu, mlango wa 14, kifungu cha 12. Na, sasa, kwa nini? Yeye alikuwa Neno. Je! hiyo ni kweli? Tena Yeye akasema, “Mkikaa ndani Yangu, Maneno Yangu ndani yenu, ombeni mtakalo.” Sasa kama mwanamke huyu ni mgonjwa, nisingeweza kumponya. Hakuna mtu angaliweza kumponya; Mungu tayari amelifanya. Ikiwa yeye ni mwenye dhambi, nisingeweza kumwokoa. Mungu amelifanya tayari; inambidi tu kuliamini.

213 Lakini sasa kama Yesu ni yeye yule jana, leo, na hata milele, na kutoa ishara ya Milele ya kufufuka Kwake, katika siku hizi za mwisho, basi Yeye angenena kupitia mimi kama mimi ni mtumishi Wake na nimeitwa kwa kusudi hili. Sasa watumishi wote hawajaitwa kufanya hivyo, unaona, lakini kuna, angalau, katika kizazi, mmoja, kwamba wanaye huyo. Sasa, lakini hili likiwa hivyo, ni la kuonyesha hao wengine, katika huduma zenu, kwamba Mungu yu pamoja nanyi.

214 Unaona, Yeye hufanya mambo mengine. Nimenena katika lugha. Sifanyi, sifanyi hivyo wakati wote. Nimelifanya mara nne au tano maishani mwangu. Sikujua nilichokuwa nikifanya. Nikijisikia mwenyewe nikizungumza siku moja, nikipata wazo, nikaangalia kote kuona ni nini kilichokuwa kinaendelea. Nikasikia mtu fulani, sauti kama kunena katika Kijerumani. Niliangalia nikaona mahali ilipokuwa. Ilikuwa ni mimi nikizungumza, mwenyewe. Unaona? Na niliwazia ningeweza kukimbia kupitia kwenye jeshi na kuruka ukuta wakati huo. Lakini nikapata, ilikuwa ni mimi, nilitulia tu kabisa mpaka Yeye akamaliza, na ilikuwa ni Roho Mtakatifu akifanya maombezi kwa ajili ya mwanamke ambaye baadaye alitokea, na akiwa mbaya sana, sana na TB, na Bwana akamponya.

215 Lakini sasa, hapa kwa kusanyiko hili, mama huyu ni mgeni. Yeye ni mwanamke mweusi, na yeye yuko mahali fulani karibu umri wangu, lakini sijawahi kumwona. Yeye ni mwanamke tu. Sasa, yeye amesimama hapa kwa sababu fulani. Sijui. Ni—nisingekuambia. Sijui chochote kumhusu. Lakini kama Roho Mtakatifu anaweza kunifunulia kilicho shida yake, ama kilichomleta hapa, ama—ama kile anachotaka, ama kitu kama hicho, ama kile ambacho amefanya, ama kile ambacho alipaswa kufanya, ama kitu kama hicho, basi, na kumwacha kuwa hakimu kama ni sahihi ama si sahihi. Je! hilo lingemshawishi kila mtu kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

216 Tutazungumza mmoja na mwenzake, kwa muda mfupi tu, maana, nyamaza, unaona. Roho Mtakatifu ni mwenye hisia sana, na ninazungumza tu na wewe kama Bwana wetu alivyozungumza na yule mwanamke kisimani.

217 Sasa, unaona, isingekuwa ni mimi, maana sikujui. Bali, unaona, mimi ni mwili wa nyama, wewe ni mwili wa nyama; lakini ndani yako kuna roho na nafsi, ndani yangu kuna roho na nafsi. Na halafu wakati Roho huyu ndani yangu, akiwa ni Roho wa Kristo, unaona, basi, na karama ambayo nilizaliwa . . .

218 Kama vile tu ungeenda kulala na kuota chochote, ungeota ndoto. Sasa, unaona, hisia hizi tano inabidi ziwe hazifanyi kazi, ndipo basi uko huku katika nchi ya ndoto. Na halafu wakati hisia hizi tano zikianza kufanya kazi tena, umeamka, unaona,

maana dhamiri yako ya ndani iko mbali sana na dhamiri yako ya kwanza.

219 Lakini wakati zote zikiwa moja kwa moja pamoja, huendi kulala, unaingia tu huko katika hiyo. Unaona? Wewe ungali katika hisia zako tano. Unaelewa? Hiyo ni karama, ambapo, ni karama ya unabii, kwamba thibitisho kuwa Kristo angali ni yeye yule. Unaona? Unaona?

220 Tuna wahudumu waliofunzwa katika Neno. Tunao tofautitofauti, watu kama Oral Roberts, ambao wanawekea tu mikono, na kuwatikisa watu, na kusema, "Bariki Mungu, wewe pokea tu hilo." Unaona, na yeye ni mmoja tu wa aina iliyo shupavu na hilo. Unaona, huyo ni mtu wa Mungu, unaona, kwa kuwa kuna aina nyingine ambao hawafanyi hivyo, bali wanafanya kitu kingine. Zote ni karama za Roho; mitume, manabii, na wachungaji. Mnaamini hilo, sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

221 Je! unaamini Mungu alinituma kufanya hayo? [Dada huyo anasema, "Ninajua hilo."—Mh.] Unajua. Asante, dada. Naam, bwana. Ni kwa nini nilikuita 'dada'? Kwa sababu, uliposema hilo, nilihisi Roho akisema hiyo ni kweli.

222 Sasa upo hapa, na ninakuona sasa; watu wangali wanaweza kunisikia. Mwanamke huyo anakosa usingizi. Hawezi kulala. Hiyo ni kweli. Ninii sana . . . unakuwa mgonjwa, pia, unakula kwa shida, unakuwa mgonjwa sana. Ninii tu . . . Na unahofia kwamba ni mawe ya nyongo. Hiyo ni kweli. Hiyo ni hakika. Uko sahihi. Mgonjwa, hisia ya kuchefukwa. Hiyo ni kweli. Basi wewe—wewe ni . . .

223 Kuna mtu mwingine ambaye unamjali. Huyo ni nanii wako, huyo ni mume wako. Na yeye ana na—na—namna ya wa—wasiwasi, wasiwasi wa akili, kwa namna fulani wasiwasi kwelikweli wa akilini. Na yeye anahangaishwa na namna fulani ya shida aliyo nayo. Anajaribu kutafuta kitu, kitu, m—mpango wa biashara, ni malipo ya uzeeni au kitu fulani anachojaribu kutafuta. Hiyo ni kweli, malipo ya uzeeni anayojaribu kutafuta. Ndilo hilo. Naam, bwana, malipo ya uzeeni. Na halafu kuna . . .

224 Ninamwona mvulana mdogo, ana umri wa yapata miaka kumi na miwili, ama kitu kama hicho. Ni jamaa mdogo tu, na kwa kweli si mwana wako. Yeye ni—yeye ni . . . Umemlea, na kuna kitu unachofikiria, kwamba, yeye, jambo fulani limeenda vibaya kwake. Yeye siye. Yeye ni mvulana mdogo tu. Atakuwa sawa. Hakika. Ni sawa. Amini kitu sahihi. Kila kitu kitakuwa sawa. Nenda, ukiamini hicho. [Kusanyiko linashangilia.—Mh.] Mungu akubariki, dada.

225 Jambo jingine, je! unaamini Mungu anaweza kuniambia kuwa wewe ni nani? Je! unaamini kwamba Mungu anaweza kuniambia kuwa wewe ni nani, mama? Bibi Red, huyo ni wewe. Hiyo ni kweli. [Kusanyiko linashangilia—Mh.]

226 Mwanangu, ni sawa. Unamjali shangazi yako. Alifikiria jambo fulani lilikuwa limetendeka, bali halijatendeka. Wewe ni mvulana mdogo tu. Hukusudii kufanya hivyo. Endelea, utakuwa sawa. Amina.

227 Jamani, jinsi Roho Mtakatifu angependa kupenya katika hilo! Unaona?

228 U hali gani? Ikiwa Roho Mtakatifu anaweza kuniambia kuwa shida yako ni nini, unaniamini basi, utaamini? [Dada huyo, anasema, "Ninaamini."—Mh.] Unaamini. Vema. Una ha—hali ya wasiwasi. Una mngurumo kichwani mwako. ["Hiyo ni kweli."] "Oo-oo-oo," kikienda namna hiyo wakati wote. Hiyo ni kweli. Halafu ulifanyiwa uchunguzi kwa ajili ya kivimbe, na wakapata kwamba kivimbe hicho kiko kwenye njia ya haja kubwa. Je! unaamini kwa moyo wako wote sasa? ["Naam."] Hiyo—hiyo ni kweli. ["Amina."] Nenda zako, ukiamini, na utapona. Amini. Umepata kile unachotaka? Vema. ["Amina."] Unaona? . . . ? . . .

229 Unaamini kwa moyo wako wote? [Dada huyo anasema, "Ninaamini."—Mh.] Kuwa tu na imani. Usitie shaka. Amini kwamba Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele. Ni mtu mwenye umri mdogo zaidi ambaye uko hapa kwa ajili yake. La, ni wawili. Unao binti wawili, na wote ni kama wana kurukwa akili, kama. Hiyo ni kweli. Bwana Mungu, warehemu watoto hao. Je, unaamini kama nitaninii tu . . . Kama nitalinena Neno Lake, unaamini kwamba watapona kutokana na huo? ["Ninajua hilo."] Basi nenda, pokea huo. Mungu akubariki. [Kusanyiko linashangilia.]

"Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana."

230 Unaamini hilo, sivyo? Unaamini kwa moyo wako wote? Je! unaamini mtoto huyo aliye na tatizo la koo atakuwa mzima? Vema, unaweza kuwa nao, bwana. Ninamwona mwanamke huyo akitokeatokea hapa ghafla, na huko nyuma, na hapa, na nikawaza, "Kilikuwa ni kitu gani?" Ameketi hapo akimwombea mtoto wake. Vema, atapona huo. Itakuwa sawa. Usitie shaka.

231 Je! unaamini kwa moyo wako wote? Unaamini kwamba Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele? Ikiwa Bwana Yesu atanifunulia kilicho shida yako, utamwamini Yeye? Una hali ya wasiwasi, matatizo; bila shaka, mwanamke wa umri wako. Bali, hata hivyo, hapa pana jambo kubwa, ni kivimbe. Je! unaamini Mungu anaweza kuniambia mahali kivimbe hicho kilipo? Kipo kwenye titi lako la kushoto. Je! hiyo ni kweli? Vema. Nenda, amini, na kitatoweka.

Kuwa na imani katika Mungu. Usitie shaka.

232 Niliona kitu cha baraka kikitendeka, na kitu cha kutisha kikitendeka, papo hapo tu. "Utii ni bora kuliko kafara, kusikia kuliko (Kitu gani?) mafuta ya kondoo dume." Je! hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Bwana Yesu, turehemu. Jamani, loo, jamani! Utii, uaminifu na utiifu; jinsi Bwana Yesu

alivyofanya tu jambo papo hapo! Ninaenda kuwaambieni katika dakika moja tu.

Amini tu. Usitie shaka.

233 Unaamini Mungu atakuponya hapo, dada uliyevalia maskini gauni la manjano, uliyeketi hapo ukiomba? Sawa, ni sawa. Vema, unaupokea.

Kuwa tu na imani. Usitie shaka. Amini.

234 Unayeketi moja kwa moja hapo nyuma katika safu hiyo ya pili, una tatizo la koo, pia, mama huyo anayeniangalia hapa moja kwa moja. Je! unaamini kwamba Yesu Kristo atakufanya mzima? Unaamini? Naam. Ilikubidi kusimama, kumpa mtu fulani nafasi kutoka. Dakika tano zaidi, na utakuwa umeponywa. Aliukosa, lakini wewe uliupata. Unaweza kuwa na haja yako sasa. Linakuacha.

235 Je! unaamini kwamba Mungu anaweza kukufanya mzima? [Dada huyo anasema, "Ndiyo, bwana."—Mh.] Je! unaamini Mungu anaweza kuniambia kilicho shida yako? ["Ndiyo."] Una kisukari. ["Ndiyo."] Mume wako yupo hapa akiwa nacho, pia, sivyo? ["Ndiyo, bwana."] Hiyo ni kweli. Nyote wawili mpate afya. Nenda, amini kwa moyo wako wote.

236 Una pumu, wasiwasi. Je! unaamini kwamba Mungu anaweza kukufanya mzima? Unaamini kwa moyo wako wote? Hebu nikuwekee mikono unapopita. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe. Jalia hilo.

237 Baridi yabisi. Je! unaamini kwamba Mungu atakufanya mzima? [Dada huyo anasema, "Ndiyo, ninaamini."—Mh.] Vema, nenda tu, useme, "Asante, Bwana Mungu. Ninaamini kwa moyo wangu wote." Naam, bwana.

238 Loo, jamani! Wasiwasi, baridi yabisi, tumbo. Amini tu kwa moyo wako wote. Endelea, useme, "Asante, Bwana, kwa kunifanya mzima."

239 Unajua, damu ndiyo mahali ambapo uhai wetu upo, sivyo? Lakini Mungu anaweza kuponya chochote (unaamini hilo?), damu, chochote kingine. Vema, imekwisha. Nenda, useme, "Asante, Bwana." Nenda, amini kwa moyo wako wote.

240 Vipi kama nilikuwekea tu mikono, na kusema, "Bwana akubariki," je! ungeamini kwamba ungeponywa? Njoo upite, basi, unaona. Katika Jina la Yesu Kristo, Mungu, mfanye mzima. Kuwa na imani.

241 Sijawahi kuona watu wengi sana hii . . . Mama huyu hapa ana baridi yabisi, pia, matatizo, vitu. Naam, hiyo ni kweli. Je! unaamini kwamba Mungu anakuponya? Vema. Endelea, useme, "Asante, Bwana Yesu."

242 Ni wangapi huko nje wanataka kuamini sasa? "Mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu."

243 Je! unaamini kwamba kinywa cha Mungu kilisema hili, ninii . . .? Yesu Kristo ni Mungu katika mwili. Tunajua hilo. Hakuna mabishano juu ya hilo. Yeye hakuwa tu nabii; Yeye alikuwa Mungu, Mungu aliyedhihirishwa katika mwili. Jambo la mwisho Yeye alilosema, kulingana na Injili, wakati Yeye alipotoka duniani, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Je! mnaamini hilo kwa moyo wenu wote? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa ni waaminio wangapi waliopo hapa, inueni mikono yenu. Vema.

244 Sasa ninataka mfanye jambo fulani. Ni wangapi hapa walio na shida fulani, ambayo wanataka iombewe? Inueni mikono yenu. Sasa, inaonekana kama ni kila mtu. Sasa, hapa ndilo ufanyalo. Wewe iweke imani yako kazini, nitaiweka imani yangu kazini, na tutafanya muungano (kunachelewa) kwa Mungu. Na halafu je! utamwombea mtu huyo walioweka mikono yao juu yako? Kwa sababu, wanaenda kuwa wakikuombea, unaona, wewe.

245 Kama, kama hapa kulikuwa na mtu, waliniwekea mikono yao, nimewawekea mikono yangu; ninawaombea, wananiombea. Ninasema, "Bwana, mimi ni mwaminio. Mama huyu, huyu mwanamume, huyu mvulana, msichana, chochote kile, anateseka. Naomba, Mungu Mpendwa. Mimi huteseka, ninajua kile wanachopitia. Waponye, Mungu Mpendwa."

246 Kuwa mwaminifu kabisa sasa, kuwa mwaminifu kabisa, na uombe tu kama vile wewe ungetaka wakuombee. Unaona? Wafanyie wengine jinsi ungewataka wakufanyie. Sasa wewe mwombee mtu huyo uliyemwekea mkono wako, vile tu ungemtaka Yesu akuombee, unaona, na uangalie kinachotukia. Unaona, Neno la Mungu haliwezi kushindwa. Je! hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ni Kweli. Hiyo, hiyo haiwezi kushindwa.

247 Sasa, sasa kitu cha kwanza tufanye, hebu tungoje tu kidogo na kukiri kutokuamini kwetu kwote. Hebu . . . Tukiri dhambi zetu zote, tukiri yote tuliyowahi kufanya, ambayo ni makosa. Hebu tuseme tu, "Bwana Yesu, nisamehe." Hebu . . . Ninataka huu uwe mkutano kwelikweli ambapo Yesu Kristo anaweza kudhihirishwa, Yesu Kristo atukuzwe. Sasa huku nikiongea na nyinyi, kirini tu kila kitu, useme, "Bwana, ni—nimekuwa na mashaka mengi. Bali papa hapa katika Uwepo Wako usiku wa leo, wakati ni—ninaposimama hapa na kuona kitu kile hasa kisichowezekana kabisa bila ya Wewe, hakuna mtu awezaye kufanya hicho."

248 Ungeona aibu kumwita "roho mwovu," maana hiyo haisameheki, unaona. Unaona, Yesu alisema hivyo. Kuita kazi ya Roho Mtakatifu, ambayo Biblia ilisema Yeye angefanya,

halafu kumwita roho mwovu, basi ni . . . basi hiyo haisameheki. Unaona?

249 Kwa hiyo unasema, "Ninasimama moja kwa moja hapa sasa, nikijua hilo, nikiketi hapa," mahali popote ulipo, "nikijua kwamba, kwamba—kwamba—kwamba Wewe upo hapa. Mbona, usingeweza kufanya mambo haya . . . Na sasa, Ndugu yetu Branham, yeye anayo tu imani kuamini kwamba Neno Lako ni kweli, na yeye ana kipawa. Ninacho kipawa, pia, kipawa cha upendo Wako. Nina kipawa cha Roho Wako ndani yangu. Nina kipawa ndani yangu, na katika kipawa hicho kuna uponyaji. Sasa, mimi—mimi ninaomba uponyaji kwa ajili ya rafiki zangu wagonjwa wanaoketi hapa. Ninaomba uponyaji, na wao wanaenda kuomba uponyaji kwa ajili yangu. Sasa Wewe nisamehe dhambi zangu. Na, Bwana Yesu, kama nimefanya au kusema chochote kibaya, nisamehe. Nifunulie, Bwana, nitaenda nikisahihishe. Ikiwa Wewe utakifunua tu na kunionyesha kile ambacho nimefanya makosa, nitaenda nikisahihishe."

250 Na ninaomba sasa kwa ajili ya rehema kwa kusanyiko hili. Tujalie, Bwana. Warehemu wagonjwa na wanaoteseka. Watu hao wapo hapa wanaomba. Wanaamini.Wamekuona Wewe ukiwepo. Nimekuona Wewe, Bwana. Sisi sote tumeona ushahidi hasa wa Mungu aliye hai.

251 Tumesahau kwa mbali. Tumeenda kwa nguvu sana, Bwana, upande ule mwingine, upande wa mbegu iliyochanganywa, madhehebu, na kanuni za imani, na makanisa makubwa, na shughuli za siku. Sisi Wapentekoste, Bwana, tumekuona Wewe ukifanya mengi, mpaka tumejifanya tu wagumu wenyewe mbali na Wewe, karibu. Ni—ni ya kusikitisha, Baba. Tusamehe jambo hili. Tumeona mengi sana wakati hilo likija pole pole kufikia hili, mpaka tumeninii, vema, tu—tumesahau kabisa hizo baraka, Bwana. Tusamehe, na utusaidie. Utafanya hivyo, Bwana?

252 Sasa turehemu, na hebu Roho Mtakatifu mkuu, aliye hapa sasa, achukue uongozi wa kila mwaminio hapa ndani. Na sasa, kama mtumishi Wako, ninaombea kila mtu mgonjwa hapa. Ni—ninakuomba Wewe, Bwana, kutia nguvu mikono itakayowekwa juu ya wagonjwa. Jalia—jalia nguvu za Roho Mtakatifu ziwe juu ya kila mmoja wa wanaume hawa, wanawake, wavulana na wasichana, tunapoketi pamoja, Bwana. Watu walioketi hapa, wagonjwa, Bwana, kwamba wataninii . . . Watoke hapa kuwa wenye afya. Jalia waje kesho usiku, wazima. Tujalie, Bwana, naomba utujalie. Yasikie maombi yangu. Ni—ninaomba kwa moyo wangu wote, kwamba Wewe utafanya hivyo, nikiungama kila kitu ninachokijua ambacho ni kosa. Na sasa utusaidie, na sasa umwache Roho Mtakatifu achukue mamlaka. Na watu hawa wakiwekeana mikono, naomba kwamba wafanywe wazima, sasa hivi. Tujalie, Baba, kupitia Jina la Yesu Kristo.

253 Na sasa, Shetani, nakuamuru, kwa Damu ya Yesu Kristo, ile Damu inayojitosheleza kwa yote; kwamba kupitia ule Uhai uliokuwa katika Damu hiyo, ambao sasa uko mioyoni mwetu, tumebadilishwa kutoka kile tulichokuwa wakati mmoja, kuwa Wakristo. Wakati mmoja tulikuwa wenye kushuku, sasa tu waaminio. Dhambi zetu ziko chini ya Damu.

254 "Yeye atakayeungama dhambi zake atapata msamaha." Tumekiri dhambi zetu, na tunao msamaha. Sasa tunasimama, bila. . .Dhambi zetu ziko katika Bahari ya Usahaulifu. Hatuwezi tena kuhukumiwa kwamba tuna dhambi. Tumeikiri. Tumesahihisha mambo. Na sasa shimo kubwa, lililokuwa kati yetu na Mungu, limeondolewa. Mungu aliweka dhambi katika Bahari ya Usahaulifu. Hata asingeweza kutukumbuka tena kama wenye dhambi. Sisi si wenye dhambi tena. Sisi ni wana na binti, na sasa tupo hapa kwa ajili ya ukombozi kwa ajili ya mwili. Na kwa sababu sisi ni waaminio, Neno lilisema, Neno, Neno ambalo Kristo alituachia, kasema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Na hili tunafanya, kwa imani tunalifanya, katika Jina la Yesu Kristo.

255 Sasa, kila mtu humu ndani, weka mikono yako juu ya mtu fulani karibu na wewe. Weka mikono yako juu ya mtu fulani karibu na wewe, na sasa useme:

256 [Kusanyiko linarudia baada ya Ndugu Branham—Mh.] Shetani, ninakuamuru. Ninakuamuru, Shetani, katika Jina la Yesu Kristo, achilia huru rafiki yangu. Toka hapa. Umeshindwa. Rafiki yangu amepona. Ninaamini Yesu Kristo sasa ananiponya, kumheshimu Yeye, kuleta sifa.

257 Amini hilo kwa moyo wako wote, nafsi yako yote, nia yako yote, na Mungu Mwenyezi atajalia hilo. Mungu awabariki.

Kuna Njia Moja Tu Iliyotolewa
Na Mungu Kwa Kitu Chochote SWA63-0731
(There Is Only One Way Provided By God For Anything)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatano jioni, tarehe 31 Julai, 1963, katika Marigold Center kule Chicago, Illinois, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2019 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org